MFANO WA TAI ATAHARIKISHAVYO KIOTA CHAKE

Asante, sana.

2 Bwana awabariki, ndugu na dada. Nina furaha sana kurudi maskanini tena alasiri ya leo, kanisa.

Mnajua, mnasema, "Vema, hili si kanisa, hili ni jengo la Legion."

3 Ni kanisa wakati Kanisa likiwa hapa ndani. Naye Mungu yuko ndani ya Kanisa Lake. Hiyo ni kweli? Mungu yuko ndani ya watu Wake, kwa hiyo watu Wake ni Kanisa Lake. Kwa hiyo sisi hapa, sote tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukifurahia ushirika uliobarikiwa, wakati Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na uchafu wote. Hilo si ni zuri sana? Huru tu wakati wowote Bwana anapotaka kutuita, tunaruka tu kidogo na kuingia moja kwa moja Mbinguni, katika yapata sekunde mbili tu baada ya sisi kuondoka. Hiyo si ni sawa? Ni hakikisho lililobarikiwa jinsi gani!

4 Nilikuwa nikizungumza siku moja katika Wafanyabiashara Wakristo huko, ninaamini ilikuwa ni Tijuana, la, samahani, ilikuwa huko—huko Jamaika, Kingston, Jamaika, nao walikuwa na watu wote mashuhuri na Wakuba wengi huko juu. Ndipo usiku huo mtu fulani akaniambia, baada ya kumaliza kuzungumza, kasema . . . Tu—tulifanya ibada zetu kwenye uwanja wa mashindano ya mbio, bali nilishuka kwenda mahali fulani pakubwa pamoja na hao watu mashuhuri, mwajua, kuzungumza usiku huo. Ndipo kasema, "Aisee," akasema, "wewe—wewe ndiye yule mhubiri hapa juu, sivyo?"

Nami nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Unafanya nini hapa chini pamoja na hawa wafanyabiashara?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyabiashara."

"Loo," kasema, "sikujua."

Nikasema, "Naam, mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Unafanya biashara ya aina gani?"

Nikasema, "Biashara ya bima."

Akasema, "Biashara ya bima ya aina gani?"

5 Nikasema, "Bima ya Uzima wa Milele." Ningali ninaifanya hiyo biashara. Sasa, kama mtu yeyote hapa angependa kuzungumzia hati ya mkataba pamoja nami, ningefurahi kuzungumza nawe wakati wowote, bima ya Uzima wa Milele.

6 Nilienda shuleni pamoja na mvulana mmoja, Wilmer Snyder, jamaa mzuri sana. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

7 . . . Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 32:11:

> *Mfano wa tai ataharikishavyo kiota chake, na kupapatika juu ya makinda yake, . . . kuwatwaa . . .* juu *ya mbawa zake*, na *kuwatwaa* juu.

8 Sasa, somo nililotoa kuzungumzia leo lilikuwa, "Tai Akitaharikisha Kiota Chake." *Mfano Wa Tai Ataharikishavyo Kiota Chake.*

9 Na kwa hiyo sitawaweka muda mrefu sana sasa, ili kuwe na wakati mnapoweza kujiandaa na kwenda kanisani. Hivi mna ibada nzuri asubuhi ya leo, kila mtu? Loo . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

10 . . . alifananisha urithi Wake na tai. Mwajua, nilianza kusoma habari za tai wakati mmoja, nami nikaona kuna yapata aina arobaini mbalimbali za tai, na yapata aina nane mbalimbali zimetajwa katika Biblia.

11 Baadhi yao, wanadai kuwa, ya kwamba baadhi yao walikuwa ni koho kwa sababu wanakula mizoga, lakini hilo lilikuwa ni kosa. Ningetofautiana tu na mtu aliyeandika, kwa sababu ninawajua tai. Tai hula tu nyama iliyo hai, koho hula—hula mizoga. Lakini tai halisi hujiulia nyama yake mwenyewe, hana budi kuila mbichi, kama tu dubu mkali wa kijivu na dubu mweusi. Dubu mweusi ni mla mizoga, yeye—yeye hula mizoga. Lakini—lakini dubu mkali wa kijivu, hana budi kuua mbichi kila usiku, ama wakati anapotaka kula, yeye hula. Na vivyo hivyo na tai, tai hula nyama mbichi. Hataki kitu chochote kilichochacha, ama mabaki, ama cha kuachiwa, yeye—yeye anataka kujitafutia nyama yake—yake mwenyewe.

12 Kwa hiyo tunakabili somo kuu, na ndege mashuhuri. Nami sikuzote nilimpenda tai, ingawa ameniletea matatizo mengi, amekula kulungu wengi ninaowaua, bali ni—ningali ninamheshimu. Yeye ni ndege mwindaji, na neno lenyewe *tai*, lenyewe, linamaanisha "anayerarua kwa mdomo," yeye hurarua kwa mdomo wake halafu anakula.

13 Na hiyo ni njia nzuri ya kuliangalia, wito wa Mungu, kwa sababu Mungu hulisha kwa kinywa Chake, nacho kinywa Chake ni Neno Lake, ambapo Neno Lake linatokea. Naye aliufananisha urithi Wake, sisi, na wanatai Wake. Na Yeye Mwenyewe ni Yehova-Tai. Mlijua hilo? Mungu anajitangaza Mwenyewe kuwa ni Yehova-Tai, Yeye Mwenyewe ni Tai. Yeye ni Baba Tai, nasi ni tai wadogo, watoto Wake.

14 Nami nimejifunza mengi kuhusu tai, nilipowachunguza, nami ni mpenda maumbile sana. Maumbile ndipo nilipomwona Mungu kwa mara ya kwanza, kumtazama. Nimeyaangalia maua nilipokuwa tu mvulana mwenye dhambi, na kuona maua madogo, jalidi ingeyapiga, nayo yangeinamisha maskini vichwa vyao, na mbegu ndogo nyeusi ingeanguka kutoka kwayo.

15 Hivi unajua wana msafara wa mazishi kwa ajili ya maua? Mliwahi kujua hilo? Hakika, Mungu ana msafara wa mazishi, bila shaka anao. Mvua za msimu wa kupukutika zinakuja, nao unalia ukadondosha chini machozi makubwa mno, yanazika hizo mbegu za maua, bila shaka huzizika. Yeye ana msafara wa mazishi.

16 Na halafu zinakaa mle, wakati wa baridi kali, mbona, ardhi inaganda, nalo hilo shina dogo linakauka, tunguu linakauka, petali zimetoweka, maskini hiyo mbegu inaganda, inafunguka, nyama yote ya hiyo mbegu inakwisha. Huenda ukachukua konzi la udongo huo, uupeleke kwenye maabara, na kuuchunguza tena, na tena, na kamwe hutapata chochote cha mbegu hiyo kilichosalia humo ndani, bali hebu tu jua lianze kuangaza. Kuna chembechembe ya uhai mahali fulani ambayo Mungu ameficha katika mbegu hiyo mahali fulani katika ardhi hiyo, kutokana na mbegu hiyo, itaishi tena.

17 Ndipo nikawazia, "Kama Mungu alifanya njia kwa ajili ya *mbegu* kuishi tena, ni zaidi sana vipi amenifanyia *mimi* njia ya kuishi tena, na *wewe* kuishi tena?"

18 Nilikuwa nikila aiskrimu siku moja nilipokuwa mlinzi wa wanyama wa jimbo la Indiana, kulikuwa na maskini mhubiri wa Kimethodisti jina lake Ndugu Spurgeon, mzee mzuri sana, Henryville, Indiana, tulikuwa tumeketi kwenye stuli tukila aiskrimu kidogo, tukifanya ushirika, na kipindi cha *Saa ya Kilimo* kilikuwa kinaendelea.

19 Maskini Kilabu cha 4-H cha Louisville kilikuwa na mtambo kule waliokuwa wameukamilisha ambao ungeweza kufanya punje ya mahindi ifanane kabisa na ile uliyotengeneza shambani. Nawe ukimwaga gunia zima la yale yaliyotengenezwa na huo mtambo, na gunia zima lililojaa yaliyokuzwa shambani, uyaweke mikononi mwako, uyachanganye, kamwe usingeweza kuyatofautisha. Uyapeleke kwenye maabara, uyakate vipande-vipande, kila moja ilikuwa na *kiasi fulani* cha kalisi, na *kiasi fulani* cha unyevu, sawa kabisa. Njia pekee ungaliweza kuyajua tena ilikuwa ni kuyazika, na yote mawili yangeoza, bali yale yaliyofanywa na mwanadamu, huo ulikuwa ndio mwisho wake, bali yale yaliyofanywa na Mungu yalikuwa na chembe hai, yakafufuka tena.

20 Tunaweza kuwa washiriki wa kanisa, tujaribu kuishi maisha mazuri, lakini, ndugu, Uzima wa Mungu ndio muhimu. Watu wawili wanafanana kabisa, wanaenda, wote wawili wanaenda

kanisani, wote wawili mashemasi, wote wawili wachungaji, mmoja ana chembe ya Uzima, na huyo mwingine hana chembe ya Uzima. Kwa hiyo tofauti ni kwamba ambapo unapata asili hiyo, kuzaliwa upya, *kitu fulani* hicho kilichoko humo ndani kinachoondoa ma—mashaka yote kwake, na kukupa hakikisho *hapa* ndani ya kwamba unajua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu roho yako, na Roho Yake ni moja, zinashuhudiana.

21 Loo, ni ajabu jinsi gani kujua neema na utukufu wa Mungu ambao umekuja kwetu na kumiminwa ndani ya mioyo yetu kwa Roho Mtakatifu! Hakuna kitu kama huo.

22 Kusoma, na kuwaangalia jamaa hawa, hawa tai, kuchunguza asili yao, mwaka mmoja huko Colorado. . . Na—napenda kuwinda, wala sipendi, mimi si mwuaji, mwindaji. Nami ninapenda tu kutoka nje, nipande juu ya mlima, niketi chini, na kuwaangalia wanyama, nione jinsi wanavyoenda.

23 Kamwe maishani mwangu, ninavyokumbuka, sijapita kiwango cha chochote, kwa sababu, nanyi wawindaji kumbukeni hilo, ni—ni dhambi kwa Mkristo kuvunja sheria, hupaswi kufanya hivyo, basi kumbukeni.

24 Nanyi wavulana wadogo mlio hapa, msiwapige risasi robini wangu. Huh-um. Hao ni wangu, mnaona. Je, mliwahi kusikia hekaya za robini, enyi wavulana wadogo? Sasa, kama unataka kuwapiga risasi shomoro wa Kiingereza, hiyo ni juu yako, na baba na mama, na kadhalika, unaona, bali robini wangu na hua, msiwapige risasi, kumbukeni, hao—hao ni ndege wangu, mnaona. Mnajua jinsi alivyopata maskini kifua chake chekundu? Ni wangapi wamewahi kusikia jinsi alivyokipata, ile hekaya?

25 Siku moja kulikuwa na Mtu aliyekuwa akifa msalabani, kila mtu alikuwa amemwacha, hata Mungu Mwenyewe alikuwa amemwacha. Mnajua kilichotukia? Maskini ndege mdogo wa hudhurungi alimwangalia pale, na akamsikitikia sana, akaangalia, mikono Yake ilitobolewa kwa misumari, na miguu Yake ikapigiliwa msalabani, alikuwa gerezani.

26 Mnajua kile maskini ndege huyu wa kahawia alichofanya? Alimsikitikia sana, akakimbia tu moja kwa moja mle na kujaribu kuichomoa misumari hiyo, na katika kufanya hivyo, maskini kifua chake kikawa chekundu kwa damu. Tangu wakati huo, amekuwa na kifua chekundu. Hutaki kumpiga risasi, sivyo? Yeye ni ndege mdogo mzuri. Mnapaswa kuyaona hayo macho madogo maangavu yakinitazama.

27 Loo, maumbile, ninakumbuka nikijifunza juu ya tai. Siku moja nilikuwa nimeketi Colorado, nami nilikuwa nikiangalia, ilikuwa ni katika kuwakusanya ng'ombe majira ya kuchipua, tukiwaingiza ng'ombe ndani, ndipo nikapanda kilimani, nami nilikuwa nikimwangalia tai, jinsi alivyokuwa akiwaleta watoto wake, na yale aliyofanya nao. Nami nikawaza, "Ni ajabu jinsi

gani!" Nikachukua darubini yangu, na kufika moja kwa moja karibu na mahali alipokuwa.

28 Halafu mwaka mmoja nilikuwa huko juu nikiwinda kulungu. Nayo theluji haina budi kuwashusha kulungu, isipowashusha, wao ni wa mwitu, hawafiki mabondeni, ambapo wakati mwingine wavuvi, na kadhalika, hupanda wakaja kwenye hivyo vijito, na lakini wanakaa juu sana. Wala hakukuwako na theluji ya kuwashusha.

29 Kwa hiyo, mimi na huyo mfugaji tulikuwa, tulikuwa tumetengana, tungeonana katika siku mbili ama tatu zijazo, nasi tungekutana ng'ambo ya mahali tulipokuwa tukiwinda, yeye upande mmoja wa kigawa mito, mimi upande mwingine. Nami nilikuwa na yapata farasi kadhaa wa mizigo, na farasi mmoja wa matandiko, kwa hiyo nikapanda juu sana ambapo sikumchukua farasi wangu mapema asubuhi hiyo, na kupanda juu, nikamfunga miguu tu, ili aweze kula kidogo, kisha nikapanda juu sana.

30 Basi katika majira ya kupukutika mwakani karibu Oktoba kule, itanyesha kidogo, na theluji ianguke kidogo. Loo, mnajua jinsi ilivyo, karibu kama Machi hapa chini. Ndipo jua litakuja na kuikausha yote. Ndipo kunatokea dhoruba, moja ya hizo za kasi za Kaskazini, na palikuwa na maskini uwazi hapo karibu, nilikuwa karibu kwenye mpaka wa msitu, nami nilikuwa ndio kwanza niingie nyuma ya mti, na kusimama namna *hii* mpaka dhoruba ilipokwisha. Ndipo baada ya dhoruba kwisha, nilisimama pale. Upepo ulikuwa baridi sana wakati ulipokuwa ukivuma, upepo ukivuma, na mvua ikinyesha, mvua ya vuli, na mimea isiyokauka ilikuwa inaganda.

31 Ndipo huko nyuma kabisa magharibi, jua likachomoza, nami nikaliona likiangaza chini, nalo likagonga kando ya mlima, majani hayo yasiyokauka yakaganda, yakafanyiza upinde wa mvua kukingama hilo korongo. Hilo jicho kubwa mno limeketi kule nyuma magharibi likiangalia kule, nikawazia, "Hilo ni kama macho ya Mungu yakienda huku na huko duniani kote."

32 Unajua, huwezi kwenda popote pasipo kuweza kumwona Mungu, iwapo tu utamtafuta, Yeye yuko tu—Yeye yuko tu kila mahali. Huna budi kumwingiza *hapa* ndani kwanza hata hivyo, kisha umwache ayatumie macho yako kutazama. Mweke *hapa* ndani, Yeye atatumia ulimi wako kunena, ninii tu, Yeye atatumia tu utu wako wote, kiasi tu utakachosalimisha Kwake, hicho ndicho kiasi anachoweza kutumia.

33 Mungu ana wakati mgumu sana kumfanya mtu ajisalimishe Kwake. Kama vile Samsoni, Samsoni kwa namna fulani alikuwa mtu wa wanawake, alisalimisha nguvu zake kwa Mungu, lakini asingemtolea Mungu moyo wake, huo alimpa Delila, na hizo tu ndizo Mungu angeweza tu kutumia zilikuwa ni nguvu zake. Basi kiasi kile tu utakachompa, hicho ndicho anachoweza kutumia

kwako. Loo, hebu na tumpe Yeye yote, tuseme, "Mimi hapa, Bwana, nichukue tu."

34 Tulipokuwa. . .Nilikuwa nimesimama pale, nikaangalia hilo, nikaona huo upinde wa mvua, nami nikasema, "Angalia hapa, Mungu yuko moja kwa moja juu ya mlima huu, Yule *pale* katika upinde wa mvua." Unamwona katika Ufunuo 1, akionekana, unajua, upinde wa mvua, akitembea katikati ya vile vinara vya taa saba vya dhahabu, akionekana mithili ya jiwe la yaspi na—na akiki, Benyamini na Reubeni, wa kwanza, wa mwisho. Nami nikaangalia huo, ndipo nikawazia, "Huo si ni mzuri!"

Yapata wakati huo, maskini mbwa mwitu wa kijivu akalia kilimani, naye mwenzake akamjibu huko chini.

Nikawaza, "Naam, kuna Mungu katika hilo."

35 Dhoruba ilikuwa imelitenganisha kundi la kulungu, kulikuwako na yapata, niliona kulungu themanini na kitu katika kundi hilo. Basi jaribu tu kupata mafahali walio wakubwa kuliko wote, kama mtu yeyote anavyoelewa. Ninawapenda kama tu vile ungewapenda ng'ombe wako, hutaki kuwaua kinyama, na, ati kwa sababu tu unaweza kuwapiga risasi, bali waondoe tu wale wazee, maana usipofanya hivyo, mbona, inadhuru kundi lako.

36 Ndipo nikamsikia fahali mzee kando akibweka, kwa sababu alipotea kutoka kwenye kundi lingine. Loo, jamani! Nena kuhusu, kama Daudi alivyosema, "Kilindi kikiita kilindi!" Nikisimama kule juu, na kumsikia mbwa mwitu huyo akilia kule, kumsikia kulungu huyu huku akibweka, kitu fulani chini *kabisa* ndani yangu kikaanza kuguna, nikawaza, "Ee Mungu!" Nikawaza, "Ni vizuri kuwa hapa. Laiti ningaliweza kujenga vibanda vitatu."

37 Nikafurahi sana, nikaegemeza maskini bunduki yangu kando ya mti, na kuzunguka, na kuzunguka, na kuuzunguka mti huo, nikipiga mayowe tu kwa sauti yangu yote, nikiruka juu chini, na kupigapiga mikono yangu huku na huko. Nikasema, "Haleluya! Haleluya! Haleluya!" kote.

38 Mbona, kama mtu fulani angalikuwa mwituni wangekuwa, wangewazia walikuwa na mwendawazimu huko nje. Nikazunguka-zunguka kile kichaka, upesi tu nilivyoweza kwenda, na kusema, "Mungu asifiwe! Mungu asifiwe! Haleluya!" Nikikimbia tu kwa nguvu nilivyoweza, maana nilikuwa nikijisikia vizuri. Sikujali mtu mwingine yeyote kuniona, nilikuwa tu—nilikuwa tu nikitoa mvuke, kama sikufanya hivyo, ningepasuka, kwa hiyo ilinibidi tu kupiga mbinja, kutoa kidogo kwa filimbi.

39 Kwa hiyo, nilikuwa tu nikizunguka, na kuzunguka, na kuzunguka kwa nguvu nilivyoweza. Baada ya kitambo kidogo nikasimama na kurusha mikono yangu juu, nikawazia, "Yule

pale, kule kwenye upinde wa mvua; Huyu *hapa* chini *hapa*, akiomboleza katika mbwa mwitu; Huyu *hapa*, akilia katika kulungu; Huyu *hapa*, moyoni mwangu. Loo, Wewe uko tu kila mahali!" Basi nikazunguka, na kuzunguka, na kuuzunguka huo mti tena. Nikawaza, "Loo, ni vizuri kuwa hapa! Laiti ningeweza kujijengea kibanda na kukaa hapa."

Ndipo nikawazia, "La, kama ilivyokuwa kwa Petro, Yakobo, na Yohana, kuna mtoto mgonjwa chini tu ya kilima," mnaona, "sina budi kushuka."

40 Kwa hiyo nilipokuwa nimesimama pale, niliona hapana shaka nilimsisimua maskini kuchakulo mdogo wa misonobari. Sijui kama ninyi Wateks-. . .Loo, hakika, mnajua, kama ni mahali pengine popote, mnao huku Teksas. Lakini maskini kuchakulo wa misonobari aliruka juu ya kisiki pale ambapo palikuwa na kishindo kikubwa, naye akaanza kuniambia mambo ya kila namna. Nadhani hapana shaka nilimshtua maskini jamaa huyo nusura afe. Nami nilikuwa nikikimbia huku na huku namna hiyo, nikaangalia kule, naye alikuwa ameketi pale akiutikisa huo mkia mdogo, ninii tu, "*Kwe-kwe-kwe! Kwe-kwe-kwe! Kwe-kwe-kwe!*"

41 Nikawaza, "Una shida gani, ewe jamaa mdogo? Ninamwabudu Mungu yeye yule aliyekuumba. Unataka kuona mengine yake zaidi? Mimi huyu hapa naenda!" Nikazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka tena. Nikawaza, "Ulionaje hilo? Kwa nini usikimbie-kimbie kidogo?"

Lakini jambo pekee angaliweza kuketi pale, na kusema, "*Kwe-kwe-kwe! Kwe-kwe-kwe!*"

42 Ndipo nikawazia, "Sasa, Mungu, umenivutia kwa jamaa huyo mdogo kwa nini, wakati nikiwa na wakati mzuri sana hapa, mimi na Wewe?"

43 Nikamwangalia, naye ana macho makubwa mno, ya kuchukiza, kwa vyovyote vile, mwajua, yanaonekana kutokeza mashavuni mwake, hasa wakati anaposisimkwa sana, naye alikuwa akiangalia chini namna *hii*, nikawaza, "Yeye haniangalii."

44 Nikaja kugundua, pepo zilizokuwa zikivuma katika dhoruba hiyo zilikuwa zimemlazimisha maskini tai mkubwa kushuka chini ya kitu hiki, chini ya uwazi huu. Huyu tai mkubwa wa hudhurungi alikuwa anakuja, akitoka pale, huyo ndiye aliyemsisimua maskini kuchakulo huyo, hakuwa akinisumbua hata kidogo, hakunijali. Kwa hiyo alikuwa akimwangalia yule tai kule chini, kwa sababu huyo tai angeweza kumnyakua kwa urahisi sana, mwajua.

45 Kwa hiyo mimi. . .Akaruka huko nje, huyu tai mkubwa, nami nikawazia, "Vema, sasa unajua nini kuhusu hilo?" Nilimwona tai huyu mkubwa akiruka huko nje, na hayo macho makubwa mno, ya velveti yakiangalia kote, mwajua. Ndipo

nikawazia, “Yeye si ni mrembo?” Amesimama kama futi kumi kutoka kwangu.

46 Ndipo nikawazia, “Mungu, kwa nini umeuvutia usikivu wangu kwa huyo tai, badala ya kuniruhusu nikimbie huku na huku, kuuzunguka mti huu? Si—sijui ni kwa nini Wewe ungeniacha nimwangalie jamaa kama huyo. Kama nikimwua tu kulungu, wala nisimfunike vizuri, angembeba aende naye. Kwa hiyo ni kwa nini inibidi kumwangalia jamaa kama huyo? Ninakuangalia Wewe hapa nje katika upinde wa mvua, kukuona Wewe hapa nje katika ninii—katika . . . kukusikia katika mbwa mwitu, na katika mambo haya yote.” Nikasema, “Ungekuwa wapi katika huyo tai? Hata hivyo, Biblia ilisema ya kwamba Wewe ni Yehova-Tai, nasi ni wana tai. Kwa hiyo sasa, sijui ungewezaje kamwe kuwa katika huyo tai?”

47 Nikawazia, “Ni—ningeweza kuona nini kuhusu jamaa huyo? Ninaweza kumwona ku—ku—kulungu, yeye ni mfalme mkubwa mno, yeye ndiye mfalme wa mwituni, hata ninamwona mbwa mwitu kwa mlio wake wa upweke, na—na ninaweza kuona upinde wa mvua, lakini jamaa yule, vipi kuhusu yeye, kitauwa?”

48 Ndipo ikawa niliona, alikuwa ameketi pale, nami nikasema, “Unajua nini?” Nikasema, “Jamani, ningeweza kukupiga risasi kama ningetaka.” Nikasema, “Ni—ningeweza kukupiga risasi, unaamini hilo?”

49 Kamwe hakunijali kamwe, aliketi tu pale, na hicho kichwa kikubwa mno kikiangalia juu, mwajua, na hayo macho yakiangalia juu kwenye anga, kisha yakaniangalia mimi. Nami nikaendelea kumwona akimwangalia huyo kindi. Mbona, nafikiri alikuwa na matarajio ya kumnyakua huyo kindi, ndivyo ninavyowazia, ama, huyo kuchakulo wa ardhini, ama, kuchakulo wa misonobari. Tunawaita kindi huko Indiana, lakini kwa kweli wao ni kuchakulo wa misonobari. Kwa hiyo yeye, nilimwona akimwangalia huyo.

50 Nikawaza, “Vema, vipi—vipi kuhusu yeye?” Nikasema, “Vema, kuna jambo moja, yeye haogopi.” Nami nikasema, “Nitaona jinsi alivyo na hofu.” Nikasema, “Unajua ningeweza kukupiga risasi?” Akaniangalia tu. Nikaanza kuinua mkono wangu kuelekea bunduki yangu, nikamwona akijongeza hayo manyoya, nikasema, “Kumbe, ninaona ni kitu gani.”

51 Mnaona, yeye alijua ya kwamba angeweza kufika kwenye kichaka kile kabla sijaweza kuigusa bunduki hiyo. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Alikuwa na mabawa mawili. Mungu alimpa mabawa mawili kukwepa hatari. Nami nikamwangalia akiyajaribu hayo manyoya, nikawaza, “Ee Mungu, ninaona mahali ulipo sasa.”

52 Mtu fulani aliniambia, “Hivi huogopi utafanya makosa, wakati mwingine, huko juu?”

53 Loo, la. Loo, la. Maadamu ninaweza kuuhisi Uwepo Wake uliotolewa na Mungu uko karibu, acha waseme lolote watakalo, haileti tofauti yoyote.

“Hivi huogopi mtu fulani angekulenga risasi?”

La, la. Huh-uh. Siogopi maadamu ninaweza kuuhisi Uwepo Wake, nguvu hizo zilizotolewa na Mungu, hivyo tu, kuuhisi tu Uwepo Wake huku.

“Hivi huogopi watakuchukulia kuwa ni mtakatifu anayejibingirisha?”

54 Tayari wamefanya hivyo, haikufaa kitu, ninaendelea tu vivyo hivyo. Kwa hiyo, haijalishi. Kuhisi tu Uwepo Wake karibu, mwajua, nione ya kwamba kila unyoya umekaa vizuri kabisa. Loo, jamani!

55 Inatupasa kufanya hesabu mara kwa mara, tuone tu jinsi kila kitu kinavyosikika. Hivi hamwoni hivyo? Ninapenda hilo. Kuihisi tu hisia hiyo ya starehe halisi, kama ninavyohisi sasa hivi. Mnaona? Yeye yuko moja kwa moja karibu sasa.

56 Basi nikawaza, “Vema, ninaona ni kitu gani. Na jambo lingine, yeye haogopi, kwa sababu anajua mahali anaposimama, anajua ni kiasi gani anachoweza kufanya, na ni kiasi gani hawezi. Naye anatumainia karama aliyopewa na Mungu kumwepusha na hatari.”

57 Na kama Mungu angeweza kumpa tai ujasiri kiasi hicho kwa silika, ni matumaini zaidi jinsi gani tunayopaswa kuwa nayo, amina, pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu juu yetu, kutuondoa hatarini? Ruka uende. Hakika, iondokee, simama tu, uliamini.

58 Hakuna haja ya sisi kuwa namna hii, kuwa wagonjwa, au kuvurugika, na kugawanyika katika madhehebu mia moja na . . . mia tisa sitini na tisa mbalimbali, na kadhalika, hebu turuke tuyaondokee. Amina. Tuyaondokee, hatufungwi na chochote, la, bali turuke mara moja.

Watu husema, “Loo, siku za miujiza zimepita.”

59 Usiamini hilo. Hisi tu hizo nguvu ulizopewa na Mungu zinazokuzunguka ambazo zilikuokoa na kukujaza kabisa na Roho Mtakatifu. Ni—ni kitu gani hicho? Dumisha—dumisha hisia zako za Roho Mtakatifu karibu nawe, hakikisha kila kitu, gia zote zinafanya kazi vizuri, zimetiwa mafuta vizuri kwa dawa ya macho, mwajua, na kadhalika, kusudi uweze kuondoka wakati ufikapo.

60 Ndipo nikamwangalia kidogo, nami nikakuta kwamba—kwamba yeye hakuniogopa, bali alininii tu, alichoshwa na maskini kindi aliyeketi pale, maskini kuchakulo wa misonobari, akifanya, “*Kwe-kwe-kwe! Kwe-kwe-kwe! Kwe-kwe-kwe!*” Alitosheka, nadhani labda kwa silika alijua ya kwamba nisingempiga risasi, kwa vyovyote vile, maana alinivutia ameketi pale.

61 Ninapenda chochote kilicho jasiri, namchukia mwoga. Ninamchukia mtu, ama, kuona mtu akiingia mimbarani na kuogopa kuhubiri imani yake. Ndugu, nakwambia, ningesema hata kama angenipiga risasi, vivyo hivyo tu. Na—nataka... Halafu kwenda ofisini, na mtu aponywe kwa nguvu za Mungu, kisha aogope kusema jambo fulani kulihusu. Mtu fulani aseme ya kwamba wao, "Naam, ninaamini Bwana ndiye Mponyaji," halafu aogope kushuhudia hilo.

62 Loo, ndugu! Ukimwonea aibu Roho Mtakatifu, Mungu hawezi kukutumia, Mungu anataka ma—mashujaa. Amina. Sisi ni wa jamii ya Simba, Simba wa kabila la Yuda. Hiyo ni kweli. Ukali, uthabiti, ushujaa. Loo, jinsi ningeweza kumfuatilia Simba huyo, na kuachia somo langu hapa!

63 Lakini juu ya—juu ya tai huyu, nilimwangalia kwa dakika chache, basi baada ya kitambo kidogo akachoshwa na kusikia hayo makelele ya *kwe-kwe*, kwa hiyo akafanya tu mruko mmoja mkubwa, naye akapigapiga mabawa yake yapata, akipigapiga mabawa yake karibu mara tatu namna *hiyo*, alikuwa amekwisha kupita msitu huo.

64 Ndipo nikawazia, "Jamani, ni mwenye nguvu jinsi gani!" Huo upepo nusura uniangushe wakati aliporuka huko juu, nguvu za bawa hilo zikipanda juu, "*Fyu! Fyu!*" namna hiyo, alikuwa moja kwa moja kwenye msitu huo. Nikawaza, "Jamani, angeweza kuruka mbali sana!"

65 Lakini mnajua nini? Kamwe hakupigapiga mabawa yake tena, la, alijua tu jinsi ya kuyaweka. Na kila wakati upepo ungeingia, angepanda juu zaidi kidogo, angeyaweka tena. Wakati pepo zingepanda juu ya hilo korongo, angepanda juu zaidi kidogo, pa—pasipo kupigapiga mara moja zaidi, akaenda zake tu.

66 Nikasimama pale, nikaanza kulia, nikawaza, "Bwana, nitashikwa na mhemko mwingine, hakika kabisa kama ulimwengu." Nami nikaangalia, huyo hapo akaenda, nami nikamwangalia mpaka akawa tu nukta ndogo nyeusi, huko *mbali* hewani. Nikawaza "Jambo ndilo hilo, Bwana. Sio kujiunga na *hili*, na kwenda kujiunga na *lile*, na kupigapiga, kupigapiga *hapa*, na kupigapiga, kupigapiga *pale* kutoka mahali *pamoja* hadi *pengine*, ni kujua jinsi ya kuweka mbawa zako katika nguvu za imani na uruke uende zako."

67 Mwache kindi huyo wa ardhini aketi hapo, akisema, "*Kwe-kwe!* Siku za miujiza zimepita. *Kwe-kwe*! Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. *Kwe-kwe-kwe!* Yote ni upuuzi, hayo yote ni mhemuko tu, hiyo—hiyo ni shauku, hakuna kitu kama hicho."

68 Loo, jamani! Weka tu mabawa yako. Haleluya! Wakati Roho Mtakatifu anapoingia kama wimbi, upande tu moja kwa moja juu Yake, namna hiyo. Endelea uondoke njiani juu Yake, panda juu, juu, juu, juu, mpaka hata huwezi kuyasikia tena. Hivyo

ndivyo, panda juu sana katika mazingira ya neema ya Mungu mpaka hata husikii hiyo *kwe-kwe* hapa, inakufa kwako, uko huko juu Mbinguni.

69 Sasa, tai alifanywa ndege wa kimbinguni, bila shaka alifanywa. Wala hakuna ndege mwingine anayeweza kumfikia. La, bwana. Yeye ni mfalme wa jamii ya ndege. Hiyo ni kweli.

Kama ninii . . . Ukizungumza, unasema, "Mwewe ana jicho la mwewe."

70 Mmesikia hilo. Ha! Yeye ni kuruta. Hajui anachozungumzia. Kama huyo mwewe kamwe angejaribu kuruka pamoja na tai huyo, angesambaratika hewani. Tai ni ndege aliyeumbwa maalum, hana budi kuwa kwa sababu anaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Vema, sasa, kama hakuwa na mwili uliojengwa maalum alipofika kule juu, angesambaratika, pia.

71 Hivyo ndivyo watu wanavyojaribu kuiga, kuwa kitu wasicho. Hiyo ndiyo inayosababisha ajali zenu zote barabarani, ninachomaanisha, kwenye barabara ya maisha, kwa sababu wanajaribu kumwiga mtu mwingine, nao hawakuumbwa hivyo, hawakuumbiwa hilo. Sijui kama hilo lilizama ndani ama la, lakini natumaini lilizama, lakini, kwa vyovyote vile. Loo, naam. Amina.

72 Tunaona, mwajua, Mmisri a—asiyetahiriwa akijaribu kuwafuata Waisraeli waliotahiriwa, walichanganuka, pia, chini ya bahari, wasingeweza kuvuka, magurudumu yao yalikwama matopeni.

73 Sasa, tunaona, kama yule tai, na kama yeye . . . Ingefaa nini . . . ? Sasa, hiyo ndiyo sababu Mungu aliwafananisha manabii Wake na tai, kwa sababu wangeweza kuruka juu sana.

74 Sasa, yeye ni ndege aliyeumbwa maalum. Na loo, manyoya yake yameshika sana hata huwezi kuyang'oa kwa makoleo. Yameshika sana, kwa sababu kama hayakushika, wakati alipofika kule juu, hayo, huko juu kwenye mazingira hayo huko juu, yeye—yeye, yangeng'oka, angeanguka tena duniani, na kuninii tu, angesambaratika.

75 Na kama mwewe akijaribu kumfuata, ama kunguru akijaribu kumfuata, angemwacha tu mavumbini. Na kwamba, kama angeenda juu zaidi, angepaa *juu sana*, huo ndio umbali angaliweza kwenda, maana yeye ni kunguru, ama mwewe, bali maskini tai anaendelea tu kupanda juu.

76 Sasa, ingemfaa nini kwenda huko juu, kama hakuwa amepewa macho ambayo yangeweza kuona mbali sana, pia? Hiyo ni kweli. Kuna faida gani kupanda juu, isipokuwa uishi juu, pia? Ishi jinsi unavyopanda, juu kadiri unavyoweza kuruka, ishi juu hivyo. Mnajua ninalomaanisha. Hilo ndilo linaloleta aibu nyingi sana juu ya kanisa, ni watu kuruka juu sana, na kuishi

duni sana, mnaona. Hilo ndilo jambo tunalopaswa kufanya, naam, kuishi juu tu kadiri unavyoruka. Hiyo ni kweli.

77 Sasa, kama tai hakuwa na sababu ya kuwa huko juu, kamwe asingeumbwa hivyo. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu Mungu alimfanya, na kumwita nabii Wake, kwa sababu nabii hupanda juu zaidi, kama vile Isaya, Yeremia, na hao wengine, walivyopanda juu *sana*. Na kadiri unavyozidi kwenda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Sasa, watu wengine hukaa tu ardhini wakati wote, kwa hiyo ono lake liko tu papa *hapa*. Lakini unapopanda juu, kadiri unavyopanda juu zaidi, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Loo, jamani! Si ajabu watu wengine hawaoni mbali sana, hawajawahi kuondoa miguu yao ardhini. Loo, ndivyo unavyoweza kuona juu zaidi!

78 Naye tai ndiye aliye juu kuliko wote, anaweza kupanda juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote, hakuna kitu kinachoweza kumfuata. Mbona, nina shaka kama ndege ingeweza kumfikia, au la. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .huko akiifanya, akitoa hewa yake mwenyewe.

79 Lakini unapoingia huko juu, ndege huyu, yule ndege aliye hai huko juu, aliangalia pande zote, anaweza kuona, macho yake yameyashinda sana ya mwewe anaweza kufika huko juu na kuona vitu. Kama vile ikiwa—ikiwa kulikuwa na dhoruba inayokuja, nawe ungeweza kuwa juu vya kutosha hewani, ungeweza kuiona kwa umbali wa mamia na mamia ya maili, kama ulikuwa juu vya kutosha, ungeweza kuiona.

80 Vema, Mungu aliwachukua manabii Wake na kuwainua juu sana, kama Yeremia, na Isaya, Yohana, na hao wengine, mpaka wakaona moja kwa moja hata kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, amina, huko mbali *kabisa*.

81 Nilikuwa huko kumtembelea ndugu fulani huko Phoenix si muda mrefu uliopita, Ndugu Outlaw. Akasema. . .Hilo ni jina baya sana kwa ndugu Mkristo, lakini yeye ni mtu mzuri, naye ni mmoja wa nanii zangu. . .

82 Ndugu Kidson, wakati mimi na wewe tulipokuwa kule, tulikuwa kwenye kanisa lake. Naye alikuwa na kwaya kule juu, walionekana kuwa wanawake wacha Mungu, wasio na rangi ya makucha usoni mwao, na walikuwa na nywele ndefu, na mavazi. Mimi—mimi daima. . .Hiyo ni nini? Ni kitu gani hicho, mnakiitaje hicho? Daima ninapata. . .Mascara. Hilo—hilo—hilo halisikiki sawa. Loo, kwa vyovyote vile, huwa midomoni, na kwenye, kote tu, mnaona. Kwa hiyo, *rangi* ndicho kilicho hasa. Vema, nakisia ndivyo ilivyo, pia, chochote kile. Vema, hata hivyo, hawakuwa wamevalia hivyo. Na maskini nyuso zao, zinametameta tu kama kitunguu kilichomenywa.

83 Nao walikuwa wamesimama pale, nao, maskini mvulana huyu amesimama pale nje akiimba, "Tunapanda juu, juu, juu." Naye akasema, "Awamu ya kwanza ilikuwa ni kuhesabiwa haki,

awamu ya pili, utakaso." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "...kutukuzwa. Ndipo Roho Mtakatifu akashuka." Kasema, "Nilianza kupanda juu, juu; juu, juu, juu; juu, juu; juu, juu, juu mpaka nikaishia kwenye Njia ya Kilimia Cheupe."

84 Nilifikiri nilikuwa nimeondoka basi, maana tulikuwa tu tukihisi...Huyo ni yule tai akipanda juu, akipanda juu *kabisa* mle ndani, unaweza kuona kule Kuja kwa Bwana.

Loo, si ajabu, wakati maskini mwanamke yule alipomwona Grant akiingia Richmond kule juu, alisema:

> Macho yangu yameuona utukufu wa kuja kwa Bwana;
> Akikanyaga zabibu ambapo zabibu za ghadhabu zimehifadhiwa.

Hakika, akishika lile ono la Kuja kwa Bwana, akipaa juu.

85 Sasa, yeye ni ndege aliyeumbwa maalum, anaweza kuruka juu zaidi, na kama akifika kule juu, anaweza kuona mbali. Naye Yehova, Baba Tai, ameketi juu kabisa Mbinguni. Loo!

86 Wakati alipokuwa hapa duniani, alipewa jina duni kuliko yote lingeliweza kutolewa, Beelzebuli; alienda kwenye mji ulio chini kuliko yote ulimwenguni, Yeriko, kisha akawa duni sana hata ikambidi kuangalia juu ya mti kumwona mtu aliye mfupi kuliko wote mjini. Hiyo ni kweli. Aliitwa kila kitu duniani, majina mabaya, kila kitu, bali alipoinuliwa, alipewa Jina lipitalo kila jina litajwalo Mbinguni na duniani, pia jamii yote, Mbinguni na duniani pia, inaitwa kwa jina Lake, Yeye ameinuliwa juu sana, hata inambidi kuangalia chini apate kuona Mbingu. Sasa, hivyo ndivyo Mungu alivyomfanyia alipofika Kule juu, hiyo ndiyo tofauti.

87 Sasa, inakubidi kushika mwendo. Sasa, sisi tuko chini tu tuwezavyo kuwa tunapokuwa wenye dhambi, hebu tushike mwendo, kuelekea Njia ya Kilimia Cheupe, tuifikie tu na tuzidi kuendelea mbele (Sasa, tunaona ya kwamba...), kupanda juu, juu, kwenda juu kwenye Ufalme wa Mungu.

88 Sasa, hawa manabii, wanapofika kule juu, wanaenda mbali sana ambapo ndege wengine wenye akili wasingeweza kuona, hawakujua, kwanza kabisa wasigeweza kupanda kule juu, bali Mungu alisema manabii Wake walikuwa tai Wake. Na sasa, Mungu alitwambia, mwajua, katika Biblia ya kwamba aliwatoa Israeli kutoka Misri kwa mbawa za Tai, hizo zilikuwa ni mbawa Zake. Loo, hiyo Nguzo ya Moto ya kuwaelekeza, Yeye aliwabeba Israeli juu ya mbawa Zake!

89 Loo, hapa muda si mrefu uliopita, tulipokuwa tukileta... Palestina ikichochewa tena, tukiona Lewi Pethrus akituma Agano Jipya milioni moja kwa wale Wayahudi waliotoka huko chini Iran, na kadhalika. Nao walikuwa wakisoma hilo Agano Jipya, wala kamwe hawakusikia juu ya kitu kama

Bwana Yesu kuwa duniani, walikuwa huko chini tangu Warumi walipowahamisha, nao wakasema, "Kama huyu ndiye Masihi, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, tutaamini."

90 Loo, ni fursa ya jinsi gani kwa huduma hii! Nikaanza safari moja kwa moja. Nilipofika Cairo, Misri, nilikuwa na ninii yangu. . .Dakika thelathini, ningekuwa Palestina. Ndipo Kitu fulani kikanigusa, nami nikaenda nyuma ya banda la ndege, kasema, "Wakati haujatimia bado." Nikarudi, nikaenda Ugiriki, kisha nikaingia India, saa ilikuwa bado. Kuwaita hao Wayahudi, wanaamini, ndugu. Naam, bwana.

91 Ndipo nikawazia, "Ni wakati wa jinsi gani wa kuwaleta hao ndugu huko nje, na kusema, 'Je, ni kweli kwamba mlisema kama Masihi huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa ndiye Masihi aliyenenwa habari zake, mnataka kumwona akifanya ishara ya nabii, mtamwamini Yeye?' Hiyo ni kweli?"

92 Nami ningesema, "Sasa, wachagueni watu kadhaa mje huku juu, tutaona kama Yeye angali ni Nabii ama sivyo, kama ndivyo alivyo. Moja kwa moja kwenye uwanja uu huu ambapo babu zenu waliukana ubatizo wa Roho Mtakatifu, sasa upokeeni."

93 Loo, basi I—Injili imeenda kwa Wayahudi, siku ya Mataifa imekwisha basi. Kitambo kidogo tu, mlango utafunguliwa, enyi wana tai, afadhali muwe mkipigapiga, na mkijiandaa kutoka hapa, kwa sababu mlango wa rehema utafungwa moja ya siku hizi. Hiyo ni kweli.

94 Loo, ni jambo kuu jinsi gani! Jinsi Mungu. . .hao. . . Walipozileta hizo ndege huko chini, nadhani mlisoma katika—katika *Reader's Digest*, la, nawaambia, ilikuwa katika gazeti la *Look*. Nina fi—fi—filamu inayoonyesha *Usiku Wa Manane Kasoro Dakika Tatu, Usiku Wa Manane Kasoro Dakika Tatu*, na ni picha ya ukubwa wa maisha ya watu kuhamia Palestina. Ndugu Arganbright, wengi wa marafiki kule chini. . .

95 Na hii. . . Walikuwa na hawa, wamewabeba hawa Wayahudi, wazee, viwete migongoni mwao. Kwa hiyo wakapanda kwenda kuwahoji, wakasema, "Mnarudi mpate kufia katika nchi ya uenyeji wenu?"

Kasema, "La, tunakuja kumwona Masihi." Hmm!

96 "Wakati mtini ukitoa matawi yake," loo, ndugu! Israeli inakuwa taifa tena kule, ile Nyota ya Daudi yenye ncha sita inapepea, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, mara ya kwanza ilipopeperushwa kwa muda wa miaka elfu mbili na mia tano, wako katika nchi yao wenyewe sasa. Hiyo ndiyo kalenda ya Mungu. Masihi atakuja, hakika tu kama wanavyosimama kule wakimngojea. Tuko katika wakati wa mwisho. Loo, enyi watoto wa tai, penyezeni kupitia mlango wa rehema, kisha mruke mwende mbio mwezavyo.

97 Walipowaleta, hizo ndege ziliposhuka kuwachukua hao Wayahudi, wangali walikuwa wakilima kwa vyombo vya kale vya mbao, kama walivyofanya mamia na maelfu ya miaka iliyopita. Wangali wanafanya hivyo Afrika Kusini. Kwa hiyo basi wakati, tunapoona ya kwamba waliiogopa hiyo ndege, waliogopa sana kuingia ndani yake, rabi mmoja mzee akajitokeza pale, na kusema, "Msiogope." Akasema, "Nabii wetu alituahidi ya kwamba siku moja tutaenda kwenye nchi ya uenyeji wetu juu ya mbawa za tai."

98 Hiyo ndege kubwa ya TWA ikaruka pamoja na hao Wayahudi, hilo ndilo nabii aliloona. Ha—hakujua ilikuwa ni nini, kama vile ungeiita ndege, alisema, "Watarudi kwa mbawa za tai," aliiona maskini hiyo ndege ikipaa huko chini miaka elfu mbili mia tano iliyopita, na sasa inatimia sasa hivi, ikiwarudisha juu ya mbawa za tai.

99 Tai huyo ni ndege, ndege kabisa! Huko kwenye Bustani ya Wanyama ya Cincinnati, ninapenda kuwapeleka watoto kule juu. Njia moja, ninachukia kuona kitu chochote kimefungiwa kizimbani, Ninasikitika sana, kwa kuwa ninawapenda wanyama pori, lakini si—sina yeyote, si hata mbwa nyumbani, maana ingenibidi kumfungia. Ninachukia kuona chochote gerezani, chochote ila nyumba ya gereza. Kuwaweka maskini wanyama hao humo ndani ili kila mtu aje na kuwakodolea macho, aangalie pande zote, nafikiri ni—ni sikitiko tu. Na halafu nafikiri kama ningekuwa tu na pesa, ningewanunua wote, niwarudishe kwenye nchi za uenyeji wao, na kuwaachilia, na kusema, "Endeleni, sasa kimbieni kwa nguvu mwezavyo, ondokeni mwende!" Silaumu . . .

100 Kundi la vitu vilivyojipaka rangi vikisimama karibu vikiwakazia macho, vikipulizia moshi wa sigara puani mwao, loo, jamani, ningechukia kusimama hapo namna hiyo, mimi mwenyewe. Aa, inapaswa kuwa tu vinginevyo, mvuta sigara anapaswa kuwa humo ndani. Yeye zaidi sana ndiye angekuwa kitu cha kufungiwa ndani, hajui vya kutosha kujitunza mwenyewe.

101 Ndipo muda si muda tunajua, nikashuka, nikamchukua msichana wangu mdogo, Sarah, tulikuwa tukitembea tumeshikana mikono, tukaenda chini walipo ndege. Basi kulikuwako na kizimba kikubwa mno kule chini, hapana shaka walikuwa ndio kwanza wamshike jamaa huyu mkubwa, alikuwa ni tai mkubwa mno, walikuwa wamemweka mle. Loo, alikuwa jitu kubwa mno, mkubwa, miguu mikubwa mno, ilionekana kana kwamba angeweza kumnyakua ndama na kuruka naye.

102 Vema, ni—nikasikia sauti ya mabawa kule chini, na manyoya yakiruka, nikawaza, "Kwani kuna nini?" Kwa hiyo mimi na Sarah tukashuka kwenda kule; alikuwa kitoto kidogo.

103 Nami ninapata raha sana kwa watoto wangu. Hivi hamuwapendi watoto? Maskini Sarah huyu, miaka michache tu iliyopita nilikuwa mkutanoni, nami nikaja nyumbani usiku mmoja, nao walikuwa wakimngojea Baba aingie. Wote wawili ni wasichana wadogo wa Baba, mwajua. Kwa hiyo wa—walikuwa wakingojea, nami sikuingia mpaka usiku sana, kwa hiyo Mama akawalaza kitandani, nami nikaingia yapata saa nane ama saa tisa.

104 Nami nilikuwa nimechoka sana kutokana na mikutano, hayo maono na kadhalika yalinichosha sana, kwa hiyo nisingeweza kulala, basi nikaamka yapata saa kumi na mbili, nikaingia sebuleni, na kuketi ki—kitini, nilikuwa tu nimeketi pale, nikiwazia juu ya huo mkutano.

105 Mara, nikasikia huko chini kwenye—kwenye chumba cha msichana huko kelele nyingi, basi—basi nikaangalia, na huyu hapa Becky anakuja, kifungua mimba changu. Kwa namna fulani ana miguu mirefu, mwajua, na—naye Sarah ni jamaa mdogo. Na kwa hiyo, huyu hapa Becky anakuja kwa nguvu alivyoweza, akikimbia tu, naye akaruka pajani mwangu namna hiyo, na kunikumbatia kwa mikono yote miwili, akaanza kunikumbatia, akipiga makelele, "Baba, Baba, Baba!"

106 Nami nikaangalia huko nyuma, mwajua, hilo linaufanya tu moyo wa mwanadamu kufurahi, basi nikaangalia, na huyu hapa dada yake mdogo anakuja, Sarah amevaa nguo za kuachiwa. Mnajua jinsi wa pili sikuzote anavyopata, miguu ya pajama mirefu *hivyo* kupita kiasi, mwajua. Alinikumbusha juu ya kanisa dogo lisilo na mipaka ya kimadhehebu, naye hu—huyo mwingine mwenye miguu mirefu alikuwako kwa muda mrefu, mwajua, kwa hiyo kwa namna fulani amekuwa hapa muda mrefu, akajua mambo mengi.

107 Kwa hiyo akanikumbatia kwa mikono yake, naye alimtangulia Sarah pale, ndipo akasema, "Sarah, dada yangu," maskini Sarah akasimama, kasema, "Ninataka ufahamu jambo hili, dada yangu, nilitangulia hapa, nami nimemchukua Baba wote, na hakuna kilichosalia kwa ajili yako." Maskini . . .

108 Hivyo tu karibu ndivyo wanavyojaribu kutuambia, hiyo ni kweli, hao wenye miguu mirefu, ambao wamekuwa huko nyuma kwa muda mrefu uliopita, mwajua, kwa hiyo, kasema, "Ninaye wote."

Kwa hiyo, kasema, "Nimemchukua Baba wote, wala hakuna kilichosalia kwa ajili yako."

"Afadhali hata mfunge milango yenu." Mnaona?

109 Maskini Sarah amesimama pale, maskini midomo yake imeinama chini, maskini macho yake meusi, machozi madogo yanatoka kwayo namna *hiyo*, nikamwangalia, nikamkonyezea jicho, nikaelekeza kidole changu, nikauchomoza mguu wangu mwingine.

110 Huyu hapa anakuja, miguu ikipigapiga kila upande, mwajua, akaruka juu ya mguu wangu. Naye kwa namna fulani, asingeweza, ha—hakuwa amechaguliwa kwa muda mrefu vya kutosha, mwajua, kwa namna fulani a—a—alikuwa shaghalabaghala, kwa hiyo ilinibidi kumfikia na kumshika kwa mikono yote miwili, la sivyo angeanguka, nami nikamkumbatia karibu nami.

111 Akanikumbatia, na kujishikilia sana kwa dakika moja, akageuka, hayo macho makubwa, mwajua, na hilo tabasamu usoni mwake, akasema, "Dada yangu, Rebekah, ninataka kukwambia jambo fulani, pia." Anasema, "Huenda ikawa ulitangulia hapa, nawe unaye Baba wote, lakini nataka ujue ya kwamba Baba amenichukua mimi wote."

112 Kwa hiyo mimi . . .? . . . Ninataka Yeye anichukue mimi wote. Sijui—sijui theolojia zote, na *D-olojia*, na ma-Ph., ma-H.H.D, na ma-Q. U.D., jambo pekee nijualo, Yeye amenichukua mimi wote, nimefunikwa *hapa* ndani. Hilo tu ndilo ninalojali, maadamu tu ninajua ya kwamba Roho Wake amenifunika katika rehema na wema Wake. Hakuna kitu ninachojaribu kustahili, hakuna chochote ningeweza kustahili, hakuna kitu ninachoweza kufanya, "Sina cha mikononi, ninaushikilia tu msalaba Wako." Bwana, nichukue mimi wote. Hiyo ndiyo njia.

113 Mimi na maskini Sarah tukienda mbele, ilikuwa siku chache baadaye, nilimshika mkono, nasi tukashuka kwenye kizimba hiki cha tai. Nami nikaona moja ya tamasha za kusikitisha sana niliyowazia nimewahi kuona, ilikuwa ni maskini tai mkubwa aliyekuwa ndio kwanza anaswe, naye ameketi katika kizimba hiki. Alikuwa amelala chali wakati nilipopanda juu, mabawa makubwa mno yametandazwa namna *hiyo*. Nikaona alikuwa akitokwa na damu kote mbele ya mbawa zake, na kichwa chake kilikuwa kinatokwa na damu kote, manyoya yameng'olewa kutoka kwake, ukingoni mwa mbawa zake, nikawaza, "Kwani maskini ndege huyo ana shida gani?"

Ndipo nikamwinua maskini Sarah na kuweka miguu yake shingoni mwangu, kusudi aweze kuona ndani ya kizimba, naye akasema, "Baba, anatokwa na damu!"

Nikasema, "Naam, labda . . . Hakuna kitu pale cha yeye kupigana nacho, sijui anapigana na nini."

114 Baada ya kitambo kidogo, akasimama, akatikisa kichwa hicho dhaifu, akageuza kichwa chake, na kuangalia namna *hiyo*. Mnajua, yeye ni ndege wa mbinguni. Akarudi nyuma kizimbani namna *hiyo*, huyu hapa anakimbia kizimbani upesi tu alivyoweza, akipigapiga mbawa hizo kubwa, na kugongesha kichwa chake moja kwa moja kwenye kizimba hicho tena, kikimwangusha kinyumenyume sakafuni, naye, damu ikitiririka kutoka kwenye mbawa zake ambapo alijaribu kukigonga

kizimba hicho apate kutoka. Kilimgonga sana wakati huo, hata akalala pale, nayo macho yake dhaifu yameelekezwa juu angani.

115 Nikawaza, "Ee Mungu, hilo si ni la kusikitisha!" Ndipo kitu fulani kikagusa moyo wangu, nikawazia, "La, hilo silo jambo la kusikitisha kuliko yote nililopata kuona, mnyama kizimbani, jambo la kusikitisha kuliko yote nililopata kuona ni mtu aliyezaliwa kuwa mwana wa Mungu," haleluya, "amebanwa na madhehebu fulani, ama kanuni fulani ya imani inayomwambia, 'Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu.'" Wakati anapokaa katika hizo kanuni za kale za kimadhehebu na kuangalia kila mahali namna hiyo!

116 Alizaliwa awe mwana wa Mungu, kanuni za imani zikamweka kizimbani, Mungu anataka atoke. Amina. Toka huko, ulizaliwa. . .Hiyo ilikuwa ni kazi ya mwanadamu aliyemweka huyo tai mle ndani, ni kazi ya mwanadamu inayowaweka ninyi watu katika kanuni za imani na madhehebu, yote ni ya ibilisi. Naam, bwana. Kumfinyilia mtu chini kwa kanuni za imani, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama furaha ya Roho Mtakatifu, hakuna kitu kama kupiga makelele, hakuna kitu kama kunena kwa lugha, hakuna uponyaji wa Kiungu." Loo, jamani! Inasikitisha! Wana wa Mungu, waliozaliwa wawe huru, kisha wakafungiwa kizimbani.

117 Ndugu, msiwadharau watu hao. Msidharau. . .Huo—huo ndio ulingo unaowafungia mle ndani, hicho ndicho kitu cha kuwavunjia. Hiyo ni kweli. Usiwadharau, wao ni. . .walizaliwa wapate kuwa wana na. . .wa Mungu, walizaliwa wawe huru. Usimwache mtu yeyote akufungie kwenye *kitu kingine* kama hicho, jambo ndilo hilo. Kaa mbali na vizimba hivyo vya kale, hiyo ni kweli kabisa.

118 Maskini tai, yeye ni ndege wa ajabu sana. Tabia zake, napenda kuangalia tabia zake, yale anayofanya. Nimewaangalia wakijenga viota vyao mara nyingi kwenye mkusanyiko wa mifugo, mwajua, tuseme, nawavalia darubini yangu, niwaangalie. Loo, ningewaangalia, mnamo asubuhi na mapema, kabla hata hatujaanza safari, ningepanda kule juu, na kuchukua darubini yangu, nione kile maskini tai huyo alikuwa akifanya kwenye kiota hicho bado. Anatoka nje, nawe unapaswa kumwona, kamwe hajengi kiota chake ardhini, tai hatajenga kiota chake ardhini, tai hujenga kiota chake juu *sana* awezapo kufika kwenye kilele kirefu zaidi.

119 Hiyo ndiyo sababu Mungu alimfananisha na Kanisa Lake, "Wewe ni mshumaa uliowekwa juu ya kilima." Hiyo ni kweli. Shauku kuu, matarajio makuu, tunatarajia mambo makuu.

Sisi si, useme, "Vema, mimi ni Mpentekoste, hilo latosha."

Hilo halinitoshi mimi, ninatarajia mambo makubwa zaidi.

"Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni wa Umoja; wa Uwili; wa Utatu," ama chochote ulicho.

Hilo haliniridhishi. Nina shauku ya kusonga mbele mpaka nitakapokutana Naye, juu, juu; juu, juu, juu.

"Nilimpokea Roho Mtakatifu, hilo latosha."

120 Halikuniridhisha, nami ningali tu ninamchukua, nikienda juu zaidi na zaidi, hiyo ni kweli, nikisonga mbele tu, juu sana, malengo makuu, matarajio makuu, malengo.

121 Sio, "Vema, tuna kanisa dogo zuri sana, tutatulia tu. Mimi na umati huu mdogo, hatutaki yeyote wa ninyi wengine kwenye kundi letu."

122 Si mimi, ninataka kunyosha mkono kwa kila kanuni ya imani iliyoanguka, ndugu, yeyote yule, nimwingize ndani. Malengo, nifanye jambo fulani. Matarajio kwa mtu ambaye amewahi kutembea katika kweli aone ukweli, kamwe hutamwingiza humo ndani hivyo kwa kumshusha chini, huna budi, wewe mkumbatie, na kumpenda, mwache ajue kwamba wewe ni ndugu, ndipo jambo fulani litatendeka. Kama wewe ni jamaa ya Yehova utafanya hivyo. Una Roho Wake. Alikuja kwa wale waliomchukia, waliomdharau, na kumtemea mate usoni Mwake, angali aliomba wangeokolewa, bila shaka. Huyo ni Roho wa Mungu ndani ya mwanadamu.

123 Sasa, sasa, jinsi tai huyo alivyo tofauti na kuku! Loo, mbona, kuku ni ndege, kama tu alivyo tai. Mlijua hilo? Mbona, ku—kuku ni ndege tu kama tai alivyo, bali kuku ni ndugu yake wa kimadhehebu, mwajua, wako tayari tu kutulia katika kanuni fulani ya imani, anajenga kiota chake moja kwa moja kwenye kitalu mahali fulani, ambapo kila panya anaweza kuingia na kukirarua, awatawanye watoto wake, wiski, wavuta sigara, wanawake wanaovaa kaptura, waliokata nywele zao, loo, kila kitu kiliwakata tu vipande-vipande.

124 Lakini tai halisi huinua kiota chake juu! Kila kitu kichafu cha ulimwengu kinaweza kuingia moja kwa moja ndani yake, lakini tai huchukua kiota chake na kuwaweka watoto wake ambao watazaliwa juu sana, mpaka hiyo pumzi mbaya hata haimpulizii. Whiu! Mnajua ninajisikia—ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi, *kwa namna fulani*, ninajisikia tu vizuri. Um-hum. Whiu! Hmm!

125 Naam, kumpandisha juu sana. Ninamwangalia, jinsi anavyochukua kiota hicho, kwanza, anaokota vijiti vikubwa mno, na kuviweka moja kwa moja chini kwenye mianya namna *hiyo*, anakijenga pande zote hivi kwamba hakuna upepo unaoweza kukisumbua. Kisha anatoka na anaokota vijiti vyenye miiba, na kukizungushia hivyo, tena, na tena, na kuvifungia ndani. Hakuna msanifu majengo nchini angeweza kujenga kimoja bora zaidi. Hiyo ni kweli. Anajua jinsi ya kufanya hivyo, huko juu *kabisa* kileleni, hakuna wanyama wala panya wanaoweza kupanda huko juu, kwa hiyo watoto wake wako salama.

126 Siku moja mwinjilisti mmoja mashuhuri alisema, "Ninaingia kwenye mji. . . " Vema, ilikuwa ni Ndugu yetu Billy Graham, nafikiri mwinjilisti hodari, aliiambia Louisville kule, akizungumza kwenye kiamshakinywa cha wahudumu asubuhi hiyo, nilikuwa kule pamoja na Mordecai Ham, ambaye alikuwa ni ndugu yangu mwema, yule aliyemwongoza kwa Bwana, aliyemwongoza Billy Graham kwa Bwana. Mimi na Mordecai ni majirani kule, kwa hiyo sisi ni marafiki wazuri sana. Naye alikuwa. . .

127 Tulikuwa tumeketi pamoja mezani, ndipo maskini Billy akasimama, akasema, "Biblia hii ndiyo kipimo!" Akasema, "Paulo alipoingia mjini," kasema, "alikuwa na mwongofu mmoja, akarudi mwaka uliofuata na mwongofu huyo alikuwa amepata wengine thelathini." Kasema, "Mimi ninaingia mjini," kasema, "nitapata waongofu elfu thelathini, nitakaporudi mwaka ujao, ama majuma mawili kuanzia wakati huo, si hata mwezi mmoja," kasema, "Siwezi kupata thelathini."

128 Kasema, "Kuna nini?" Sasa, haya ndiyo aliyosema, alisema, "Ni ninyi kundi la wahubiri wavivu, mnaketi huko nyuma huku mmeweka miguu yenu juu ya dawati na kuwatumia kadi, badala ya kuwasiliana nao kibinafsi."

129 Nilivutiwa na ninii yake—nilivutiwa na ninii yake. . .lakini hilo silo. Nikawazia: "Nataka kukuuliza jambo fulani: 'Ni nani huyo wa kibinafsi kwenye. . .? Paulo hakurudi, alimwacha tu huyo mwongofu, hivyo tu. Jambo ni kwamba, Billy, huwapeleki *mbali* vya kutosha hadi wasiyaone mambo haya yote.'"

130 Hivyo ndivyo ilivyo. Acha hao elfu thelathini wapate ubatizo wa Roho Mtakatifu, kisha urudi katika siku thelathini, uone jinsi. . .?. . .Naam. Naam, bwana. Wanawapulizia tu kanuni ndogo ya imani, wanawatoa nje, na kusema, unawaonyesha jina lako, "Hima, chukua barua yako kutoka kwa lingine, uiweke hapa."

131 Hilo silo, ondoa dhambi maishani mwako na jina lako na liandikwe kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo Utukufuni *huko* juu, ndipo ubatizo wa Roho Mtakatifu ushuke, ndipo utaruka kama tai. Hiyo ni kweli. Utatoka juu ya harufu hii yote ya kale tuliyo nayo ya kupiga makelele hapa duniani. Ni kweli kabisa.

132 Siku moja mimi na mzee mfugaji mmoja tulikuwa pamoja, tumekuwa washirika kwa muda mrefu, kamwe nisingeweza kumwongoza kwa Kristo, tulikuwa huko juu *sana* mlimani. Kidogo alikuwa na nundu ndogo mgongoni mwake, naye alikuwa amebeba bunduki kubwa mno ya fahali mgongoni mwake, akitembea huku na huku. Nu—nuru ilikuwa ikiangaza kupitia kwenye hiyo miti ambapo karibu hakuna mtu aliyewahi kutembelea, akasimama mara moja, akaangalia kote, akasema, "Hii inaonekana kama kanisa kuu la dayosisi."

Nikasema, "Jeff, nilimhisi Yeye hapa ndani tangu nilipovuka hiki kilima."

133 Akanikumbatia, akasema, "Billy, ninataka kumwona papa hapa katika kanisa Lake kuu." Jambo ndilo hilo. Akatokea... Hakuvuta sigara kamwe, wala chochote kile, naye alichukia motokaa kwa sababu alikuwa mfugaji, akasema, "Husikii harufu ya gesi, wala sigara huku juu, sivyo, Billy?"

Nikasema, "La, hapa ndipo anapoishi, Jeff, hii ndiyo sababu mimi huja hapa."

134 Panda juu! Hiyo ni kusema, inakubidi—inakubidi kufanya hivyo katika mazingira ya kiroho, usikae hapa chini kama kuku, hebu ruka umwache, uondoke.

135 Kuku, kila maskini panya anayetoka kwenye banda atamkamata, naam, bwana, usipolipeleka jambo hilo mbali zaidi ya, "Jiunge tu na kanisa, na uje kila Jumapili, nasi tutakuwa na mchezo mdogo wa karata, nasi tutacheza kroketi kwenye uwanja wa nyuma."

Hivyo sivyo ilivyo, ndugu.

"Tunywe supu ya jioni na kumlipa mchungaji wetu. Nanyi nyote mvae nguo zenu za kuogelea, mwende mkaogelee, mkabambushwe na jua."

136 Mnahitaji kubambushwa na mwana. Nina wasichana wawili, huenda wakajaribu hilo moja ya siku hizi, nao watapata mbambusho wa mwana, lakini si j-u-a, m-w-a-n-a wa Bw. Branham, mimi nikiwa na kijibao cha pipa nyuma yao, nikiwapiga mijeledi kwa nguvu tu niwezavyo kuwapiga. Hicho ndicho wanachohitaji, ni kubambuliwa kwa namna hiyo. Hmm! Naam, bwana. Loo, jamani!

137 Tunachohitaji leo hii ni uamsho mzuri wa Mtakatifu Paulo, na Roho Mtakatifu wa Biblia kurudi kanisani tena. Sawa. Matarajio yake ni makubwa. Kuku hukaa chini ardhini, anajenga kiota chake, ndipo kila panya, nyoka, na kila mla mizoga aliyepo anaingia, anakula mayai kabla hata hawajazaliwa, hata kuanguliwa. Hiyo ni kweli.

138 Hiyo ndiyo sababu Billy anawapoteza waongofu wake wote. Hiyo ni kweli kabisa. Kila panya nchini, kila maskini mvuta sigara, mcheza dansi, kila kitu kingine kinachoingia, kinawatoa. Acha ajenge kiota hicho juu kidogo huko juu wakati mwingine aviinue juu kidogo tu. Ondokeni mahali wanapoweza kuwafikia!

139 Yesu alisema, "Ukiipenda dunia, mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Yohana alisema hivyo. Watoe katika mambo ya ulimwengu. Wapeleke wasikoweza kufikiwa nayo. Na mtu aliyewahi kumwonja Yesu Kristo, ulimwengu umekufa kwake.

140 Nina Biblia ndogo nyumbani, moja ya zile zangu za kwanza, nami niliichukua hivi majuzi na kuiangalia, nilikuwa huko

nyuma, watu waliendelea kuniuliza maswali, akasema, “Je, ni vibaya kuvuta sigara?” Hapo ni wakati nilipokuwa katika kanisa la Kibaptisti. Kasema, “Je, ni vibaya kuvuta sigara? Je, ni vibaya kunywa pombe?” Nilikuwa nimeandika shairi dogo mle ndani, nami nikasema:

> Usiniulize maswali ya kijinga.
> Amua tu hili niani mwako,
> Kama unampenda Bwana kwa moyo wako wote,
> Huvuti sigara, hutafuni tumbaku, wala hunywi pombe haramu.

141 Kwa hiyo, nafikiri hilo lingali ni zuri. Hiyo ni kweli. Ungewezaje kula kutoka kwenye pipa la takataka ukiisha kula kutoka kwenye meza ya Mungu? Hakuna kitu kama hicho, kwa hiyo huwezi kulifanya. Bila shaka.

142 Sasa, kitu kingine alichomfananisha tai . . . Loo, ana mambo mengi sana, bali hatuna wakati wa kuyafikia yote. Lakini jambo lingine tai huurudisha ujana wake. Mnajua Zaburi ilisema hayo . . . Mithali ilisema hayo. “Mfano wa tai arejeshavyo ujana wake,” anaufanya upya ujana wake, anaufanya upya ujana wake. Maskini tai mzee, mara moja moja, manyoya hayo yote yanaanguka, ndipo anaufanya upya ujana wake tena, vema, hilo linafananishwa na Kanisa Lake.

143 Ninakumbuka mara ya kwanza niliyopata kuona Wapentekoste. Ilikuwa huko juu maskanini, Ndugu Raugh, hapa juu Indiana. Mimi . . . Michigan, hapo ndipo, Dowagiac, karibu na Dowagiac. Loo, ninasahau jina la mahali hapo sasa. Loo, jamani, ilikuwa huko Indiana, pale moja kwa moja mpakani mwa Michigan, na, Mishawaka, Indiana. Hiyo ni kweli, Mishawaka.

144 Nami nikaingia mle ndani, nao walikuwa na yapata wahubiri sitini jukwaani usiku huo, ndipo kasema, “Wahubiri wote waje huku juu.” Kwa hiyo nikapanda juu, nami nilikuwa Mbaptisti, na kwa hiyo, nikaketi chini.

145 Na kwa hiyo, walikuwa wamewasikia baadhi ya hao wahubiri, hao jamaa vijana siku hiyo, wote wakihubiri jinsi Yesu alivyokuwa, na jinsi Yeye alivyokuwa Mwokozi wa ajabu, na kadhalika. Basi usiku huo kwa ajili ya ujumbe mkuu, walimleta mzee, mtu mweusi huko nje, na maskini jamaa huyo, karibu ilimbidi aongozwe atoke nje. Alikuwa na koti kubwa kuukuu, la samawati, lililochakaa, la Prince Albert, likiwa na mmoja wa ukosi huu hapa juu yake, koti la kale la mhubiri, mwajua. Alikuja huko nje, mzingo mdogo tu wa nywele nyeupe, huyu hapa anakuja mimbarani namna *hiyo*. Nami nikawazia, “Vema, kwa nini wasiwaweke baadhi ya hawa vijana wanatheolojia huko nje, walete ujumbe?”

146 Maskini jamaa huyo mzee akaja nje pale, mwajua, kisha akaenda mimbarani, namna *hii*, akasema, "Mimi taka kuchukua somo langu usiku wa leo," kasema, "kutoka kwa Ayubu." Ninaamini ni 7—7:37, ama kitu kama hicho. Kasema, "Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya dunia, imekazwa wapi, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?"

Nikawaza, "Kwa nini walimweka mzee huyo huko nje kuhubiri?"

147 Basi hao jamaa wote walikuwa wakihubiri yale Yesu aliyofanya hapa chini, akaanzia huko nyuma kabla ya Umilele kuanza, akampitisha kote angani, na kumshusha kwenye upinde wa mvua ulio mlalo katika kule Kuja Mara ya Pili.

148 Yapata wakati huo Roho Mtakatifu akamgusa, akasema kwa sauti kuu, "*Whoopii*!" akaruka na kwenda akicheza dansi namna *hiyo*, kulikuwa na nafasi maradufu kuliko ilivyo hapa, akaondoka jukwaani, akasema, "Hakuna nafasi ya kutosha hapa juu kwangu kuhubiri," akaondoka pale, mwajua, jukwaa lile.

Nikasema, "Jamani, hilo ndilo ninalotaka! Kama itamfanya mzee kutenda hivyo, ingemfanyia nini kijana...?..." Hiyo ni kweli.

149 "Kama tai aurejeshavyo ujana wake." Naam, bwana. Uamsho huondoa na kutikisa hisia zote za kigeni kutoka kwako, ukaruka ukaingia kwenye angahewa huko ng'ambo. Alifananisha urithi Wake na tai, kwa sababu tai huurejesha ujana wake.

150 Sasa, inamfanya apaze sauti. Hebu angalia kanisa, litakuwa limeketi, lote limekauka kabisa, muda si muda mwajua, Roho Mtakatifu anawagusa, ninii yao...Mbona, wazee wamesimama tu kwa miguu yao, wakiruka, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu, wanafanya upya ujana wao tena hiyo ni kweli, wanafanya lolote kijana awezalo kufanya, kuruka tu, na kupiga makelele, na kupiga mayowe, na kupaza sauti; anaurejesha ujana wake. Hiyo ni kweli. Ninaamini hilo, nanyi je?

151 Kulikuwa na mkulima huko Indiana, mmoja wao alikuwa, alikuwa ni mkulima mzuri, vibanda vyake havikuwa vizuri sana, loo, nyufa kwenye vibanda, na kadhalika. Halafu kulikuwa na mkulima mwingine kule chini, ila alikuwa na pesa nyingi sana, kwa hiyo akajenga banda zuri sana ulilоweza kuona. Hili ni zuri kwa wahubiri. Kwa hiyo nasema, alijenga banda zuri kuliko yote ulilowahi kuona, alikuwa na matrekta na kila kitu, lakini jamaa huyo alikuwa mvivu sana kulima.

152 Kwa hiyo kila mmoja wao...Basi huyo mkulima mwingine, yule mkulima aliyekuwa na hicho kibanda kibaya, ile misheni ndogo mahali fulani, alikuwa na...alikuwa ni mkulima halisi, mchapa kazi, kwa hiyo alikuza nyasi nyingi nzuri za alfalfa, na kadhalika mwaka huo, na kuziweka akiba.

153 Ndipo basi, kule kwenye kibanda mwaka huo, vibanda vyote viwili, ndama alizaliwa. Basi majira ya kuchipua yaliyofuata upepo wenye joto ukaanza kuvuma, walimwachilia, yu—yule mkulima tajiri kule chini akamwachilia ndama wake mdogo, maskini jamaa mdogo, amekonda sana, akatoka akiyumbayumba, pepo karibu zimpeperushie upande mmoja, ilikuwa vigumu kwake kutembea. Hakuwa na chakula, kulikuwa na magugu ya kale kule juu, mwajua, magugu ya kale, ya kimadhehebu. "Sisi ni *hiki-na-hiki*. Sisi ndio watu wakubwa." Hilo kamwe halitamnenepesha mtu, la, la.

154 Lakini huyu ndama mwingine mdogo, hakuwa na banda kubwa la kukaa ndani, lakini, ndugu, walipomwachilia, alikuwa amejaa vitamini, na mnono, jamani, mviringo na mnono tu alivyoweza kuwa. Jamani, alirusha tu mateke yake, na kuanza kuupiga upepo huo, mwajua, akaupiga, naye alikuwa tu—alikuwa tu na ninii, wakati huo upepo wa nguvu ukienda kasi ulipomgusa, alikuwa tu na wakati mzuri, akikimbia tu huku na huku, akirusharusha visigino vyake.

155 Mnajua kile maskini ndama huyo mdogo alifanya? Akakichomoa maskini kichwa chake kwenye ufa wa ua, akasema, "*Tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk*! Ulokole mtupu!"

156 Shida ilikuwa ni nini? Alikalishwa njaa sana kwa magugu ya kimadhehebu. Tunachohitaji ni vitamini za Roho Mtakatifu kanisani, zitarejesha ujana, utawarejesha vijana wa kanisa, uwarudishe kwenye Pentekoste tena, uwaletee tukio, amina, mnenepeshwe.

157 Tunaweka mengi kupita kiasi, na hiyo ndiyo shida yetu sisi Wapentekoste, tunaweka mengi kupita kiasi kwenye majengo yetu siku hizi, na kudai Yesu yuaja. Naam, bwana. Tunachopaswa kufanya ni kuingia kazini, huko nje tukimleta mtu mle ndani, tukiokoa nafsi, tukiwalisha vitamini za Mungu kupitia nguvu za Mungu. Hiyo ni kweli kabisa.

158 Sasa, hatimaye maskini yule tai anachukua mahali kuninii. . .mimi. . .Mambo kadhaa kumhusu, lakini sina budi kugusia tu mambo muhimu sasa, muda wangu unakwisha. Kwa hiyo sisi. . .Hebu tumwone akijenga kiota chake. Yeye atakuwa na, watakuwa na kiota kilichojaa vifaranga. Anajenga kanisa lake, mwajua, huko juu kabisa juu ya kilima, na kulikaza vizuri sana.

159 Sasa, kiota hicho kimejaa miiba. Vema, hataki kitu hicho, hutaki waongofu wako wapya wajue miiba yote kwenye kitu hicho, wajua, jinsi ilivyokubidi kupigana vita kufika kule. Lakini mnajua yale tai afanyayo? Anatoka na kuweka vitu vyororo kwenye kiota hicho, unapaswa kukiona. Maskini huyo mama tai atatoka na kuchukua ngozi ya sungura, amle huyo sungura, kisha achukue ngozi, na kuziba kila ufa mdogo namna *hiyo*, akifanye tu mahali padogo, palipojaa manyoya, loo, kiota

kizuri sana, kidogo, cha starehe kwa ajili ya vifaranga kuzaliwa ndani.

160 Hivyo ndivyo Mungu anavyolifanya, mwajua. Loo, jamani! Wakati—wakati unapookoka kwa mara ya kwanza, hivi hujisikii vizuri, ukitembea kwenye maskini sufi hiyo, nzuri, mwajua, loo, jamani, hiyo miguu midogo, laini, mwajua, vizuri tu. Loo, hilo ni zuri sana!

161 Loo, jinsi baba anavyotembea huku na huko kwenye hicho kiota basi, hao watoto wadogo wanazaliwa, akiwaangalia. Hmm! Jamani! Loo, umewahi kumwona akienda kwa mkogo, akitupa mabega yake nyuma na kwenda kwa mkogo, akiwaangalia watoto wake.

162 "Wote wanafanana tu na Mimi." Hiyo ni kweli. "Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Je, mnaweza kukinywea kikombe cha mateso, kudhihakiwa, kuitwa Beelzebuli, kama Mimi?"

"Naam."

"Mwaweza kubatizwa kwa Roho ninayebatizwa naye?"

"Naam."

"Kama tu Mimi." Akiwaangalia watoto wake, mnaona. Loo, jinsi anavyopiga hatua kwa mikogo!

163 Sasa, vipi kama kwa ghafla mmoja wa hao jamaa wadogo angekuwa kunguru, aruke juu ya kiota, na kupiga makelele, "*Koo*, *koo*, *koo*, *koo*"? Huh! Huyo angekuwa ni chotara.

164 Hiyo ndiyo shida siku hizi, tuna machotara wengi sana wa koho na kunguru kwenye kiota, wala si tai halisi wanaoamini, dini chotara nyingi kupita kiasi, wakijaribu kuchanganya mafuta na maji pamoja, hayatachanganyikana.

165 Mnajua ingekuwaje? Kama maskini kunguru huyo angeruka juu pale, na kupaza sauti, "*Koo*, *koo*, *koo!* Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, yote haya ni ulokole," Yeye angemfukuza kutoka mle.

Ingekuwaje kwake huko juu kwenye kiota hicho basi? Angesambaratika, kabla hajashuka chini miongoni mwa kuku, hakika angesambaratika. Naam, bwana.

166 La, bwana. Baba Tai, wanafanana tu na Yeye, wanaamini jambo lile lile analoamini, wanafanana Naye. Naam, bwana. Wameumbwa kama Yeye, wamejengwa kama Yeye, Naye anajua wao ni tai halisi. Loo, jamani! Hicho ndicho Mungu anachotaka, Masihi mdogo wa kweli. Um-hum.

167 Yeye ni Masihi. *Masihi* ni "Aliyetiwa Mafuta." Nasi ni watoto Wake, ambao tuna upako mdogo, ndivyo tulivyo, kama vile Yehova-Tai alivyo Tai mkuu, nasi ni tai wadogo, Yeye ni Masihi, nasi tukiwa na upako ule ule ni Masihi wadogo. Amina. Aliyetiwa mafuta, *Masihi* maana yake ni "Aliyetiwa Mafuta."

Je, umetiwa mafuta? Amina. Kwa kitu gani? Roho yeye yule aliyetiwa mafuta kwaye. Tunaye kwa kipimo, Yeye anaye bila kipimo. Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, nasi ni wana wa Mungu, sehemu Zake zilitoka, naam, bwana. "Kazi zenyewe nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya."

168 Huenda nikachukua kijiko kimoja cha maji kutoka kwenye bahari hii hapa nje, na kamwe hungeyakosa baharini. Hivyo ndivyo tungekumbukwa kama ingetokea tumeondoka. Lakini kumbukeni, kemikali zile zile zilizo katika bahari nzima ziko kwenye kijiko hicho, maji yale yale, hiyo ni zaidi yake tu huko nje, kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Ni . . .

Loo, unasema, "Yale ni nini *huko* nje?"

"Maji ya bahari."

"Haya *hapa* ni nini?"

"Maji ya bahari." Kweli kabisa.

169 Hivyo ndivyo Baba Tai anavyowawazia watoto Wake, jinsi anavyoenda kwa mikogo, atawapigia kelele, watajibu kwa makelele, jambo ndilo hilo.

"MIMI NDIMI aliyekuwako!"

"Amina, Baba!"

"MIMI NDIMI aliyeko!"

"Amina, Baba!"

"MIMI NDIMI ajaye!"

"Amina, Baba!"

"MIMI NDIMI yeye yule jana, leo, na hata milele!"

"Amina, Baba!"

"MIMI ningali Mponyaji!"

"Amina, Baba!"

"Bado ninatoa Roho Mtakatifu!"

"Amina, Baba!"

"MIMI ni yeye yule jana, leo, na hata milele!"

"Amina, Baba!" Amina.

170 Maskini kunguru mdogo anasema, "*Koo, koo, koo!*"

171 "Ewe koho, unapiga makelele ya nini? Toka kwenye kiota!" Maskini koho, usingeweza kula chakula cha tai, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli. Loo, jamani!

172 Ndipo muda si muda mwajua, anakuta kwamba wao ni— wao ni wazima, maskini tai wadogo, anatembea huku na huku. Na muda si muda mwajua, Mama amekusudia ya kwamba ninii yake—ya kwamba maskini tai wake hawatakuwa kama kuku wa ardhini, hawatatembea juu ya hiyo wakati wote, atawapa

majaribu machache aone jinsi watakavyotokea. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa, kujaribiwa.”

Na wanaporudi nyuma, wanasema, “La, ninapaswa . . . ”

173 Loo, mbona, kwanza kabisa wewe hukuwa mwana. Kama huwezi kustahimili kurudiwa basi Biblia ilisema unakuwa mtoto haramu, wala si mwana wa Mungu. Kwa hiyo hivyo ndivyo unavyowatofautisha.

174 “Kama mtu alivyotoka akaenda,” Yeye alisema, “Ufalme wa Mungu, akatupa jarife baharini, na wakati alipolivuta, alikuwa na terapini, kamba wa maji baridi mijusi, na kadhalika. Akawavuta ukingoni.” Hiyo ni kazi ya mhubiri, hatujui yupi ni yupi. Baadhi yao ni samaki, baadhi yao ni mijusi, baadhi yao ni nyoka, baadhi yao ni kamba wa maji baridi.

175 Mwangalie maskini kamba wa maji baridi wakati akiwa pale, mtu fulani aseme, “Utukufu! Haleluya! Bwana asifiwe!”

Unasema, “*Blump*, *blump*, *blump*, *blump*, *Blump*, *blump!* Siwezi kuamini hilo,” huyo anarudi moja kwa moja majini.

176 Maskini nyoka anainua tu kichwa chake, asema, “Nilidhani nilikuwa kanisani, lakini ni watakatifu wanaojibingirisha,” naye huyu hapa anaondoka.

Alikuwa nini? Nyoka kwanza kabisa, kwanza kabisa ni kamba wa maji baridi.

177 Maskini bibi buibui, *plunktu-plunk*, anarudi moja kwa moja kwenye shimo la matope tena, moja kwa moja anatoka, amevaa kaptura, anakata nywele zake. Naam. Sawa. “Kama nguruwe aendavyo kwenye kugaagaa kwake, mbwa kwenye matapiko yake,” haya basi. Usikasirike sana, kaa tu kimya.

178 Nilipokuwa mtoto mdogo tuliishi huko Kentucky, nasi tulikuwa na maisha magumu. Mama alikuwa akichukua maskini ugali wa mahindi, sijui kama mnajua ni nini au la, njegere jicho jeusi na mboga za tanipu,‘ na wakati angechukua maskini ugali huo, hatukuwa na mafuta ya nguruwe, angeyeyusha ngozi za nyama, na kisha angeifanya hiyo, grisi, iliyotoka kwenye ngozi za nyama iwe ni ya kupaka huo ugali.

179 Nanyi mwajua, kidogo yalikuwa ni maisha magumu. Kwa hiyo, kila Jumamosi usiku sote tulikuwa tukioga kwelikweli, nasi tulikuwa na beseni kubwa ya mwerezi, kisha wanamwaga maji mle ndani na kuyachemsha, tulikuwa kama tisa, na kwa hiyo wote wangeoga, kamwe hukubadilisha hayo maji, ni kuongezea tu maji mengine ya moto, nilikuwa wa mwisho aliyepaswa kuoga, jamani, nilioga kweli.

180 Lakini, halafu basi, jambo ni kwamba baada ya hapo, kujiandaa kwa ajili ya shule ya Jumapili, sasa, hii ilikuwa Jumamosi usiku, na Jumapili sote tungekunywa kipimo kizuri cha mafuta ya mbarika kwa sababu ya jinsi ilivyotulazimu kula. Yalinichefua, ningeshikilia pua yangu, niyagugumize tu,

nikasema, "Mama, hata siwezi kuvumilia kitu hicho." Ningali siwezi.

Akasema, "Mpenzi, kama hayakuchefui, hayakufai kitu."

181 Hivyo ndivyo Injili hii ilivyo, kama haichochei kabisa ulaji wako wa kiroho, ikuchefue sana, hutaenda kuchimbua na kutafuta kujua kama ni kweli ama si kweli. Sawa. Naam. Loo, naam. Ni—ni nzuri kwenu, itawachochea nyote, na kuwatengeneza, kuwafanya tayari kwa ajili ya U—Unyakuo utakapokuja. Hiyo ni kweli. Naam.

182 Kwa hiyo mama huyu ameamua hataki vifaranga wake wa tai wawe tu kuku wa kimadhehebu. Jamani, la! Ameamua hivyo, kwa hiyo hana budi kuwatoa kwenye kiota hicho. Wakati kila kitu kinafanya kazi vizuri, hana budi kuwafanyia majaribio. Kwa hiyo mnajua anachofanya? Anaingia moja kwa moja mle ndani, na kuchukua mdomo wake mkubwa, yeye na baba, na kutupa nje kila moja ya ma—mabunda hayo kutoka mle, ndipo kinaparuza, loo, jamani, kama ilivyokuwa baada ya Pentekoste. Mateso yalitokea, na kadhalika, mwajua. Kila wakati maskini tai mdogo anapoanza kuketi chini, angeruka, alikalia mwiba. Je, umewahi kuwa na tukio hilo? Kila mahali uendapo, miiba.

183 Sitaki kuuzoea ulimwengu, hutaki kuuzoea, la, la, na kutembea juu ya vitu laini. Loo, jamani! Hebu tushike njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Hiyo ni kweli.

184 Maskini tai mdogo kwa namna fulani alipata . . . Yeye—yeye alifanya hivyo makusudi, kusudi asije akazoea kiota hicho, yeye ni tai, yeye si kuku. Anataka kumpeleka huko nje kusudi aweze kuwaamini walio wake. Ili kwamba yeye, baada ya kitambo kidogo, kamwe asiweze tu kuketi chini, ana wakati mgumu sana. Ndipo mama anaamua basi kwamba anataka kumfanyia . . . anajua yeye ni tai, anamtazama, naye anaona, "Naam, yeye ni tai." Kwa hiyo, yuko tayari kuondoka kwenye hicho kiota sasa, hajaridhika na maskini mambo haya ya ulimwengu.

185 Kwa hiyo, muda si muda mwajua, akasema, "Sasa, kama yeye ni tai, kama akikaa hivyo wakati wote, atakuwa kuku. Kwa hiyo sina budi kumtoa hapa, na kumpa ujuzi fulani." Kwa hiyo anashuka juu ya kiota, anakunjua mbawa zake kubwa mno. Loo, mnapaswa kuliona! Jamani, baadhi ya hao tai wanaenea futi kumi na nne kutoka ncha hadi ncha. Angerusha hayo mabawa makubwa namna *hii*, na kupiga mayowe, "*Koo! Whaaw*!" mlio huo mkubwa, namna hiyo, angeyatikisa hayo mabawa makubwa.

186 Hao tai wadogo wamelala namna *hii*, upepo huo ukipepea namna hiyo. Jamani, wakati alipoyachambua hayo mabawa makubwa namna hiyo, sasa, hana budi kuondoa manyoya yote yaliyolegea kutoka kwao, maana usipofanya hivyo, watakufa watakapofika kule juu, yata—yataninii, hayo manyoya yatachomokea huko juu, vema basi, yako katika hali mbaya.

187 Na hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, linahitaji kuvurugwa kabisa kwa kiota, kutoa ndani yake baadhi ya manyoya yaliyolegea, kutoka kwenye mbawa hizi, naam. Ukibeba hasira na vinyongo, na mambo kama hayo, utafia safarini.

188 Mungu anawezaje kuwa na kanisa lenye ishara, na maajabu, na miujiza, mnapogombana ninyi kwa ninyi, "Mimi ni *hiki*, mimi ni *kile*," na vinyongo, na kadhalika. Jipepeeni sana mpaka Roho Mtakatifu ashuke kama upepo uendao kasi, apeperushe tofauti zote, na umadhehebu, maskini manyoya yote madogo, yaliyolegea, "Mimi ni *hiki*, na mimi ni *kile*," wewe si kitu unachopaswa kuwa, jinsi Maandiko yalivyosema.

189 Yapeperushe manyoya yote yaliyolegea, loo, jamani, yakazeni, kwa sababu atawapeleka kwenye safari halisi hivi karibuni, safari ya mtu binafsi. Loo, jamani, safari hiyo ya mtu mmoja, ya kwanza! Ndipo yeye—yeye anayapeperusha manyoya yote, nacho kiota kinachemka tu namna hiyo, hayo manyoya yaliyolegea yakiruka, kila mahali. Anaacha manyoya yarushwe nje, ili wapate mazuri yaliyokazwa mle ndani, kisha anawachunguza tena aone kama wako tayari.

190 Hivyo ndivyo Mungu anavyojaribu kulifanyia kanisa Lake sasa, kamwe hawezi kumfanya tayari, huku hayo manyoya yakiendelea tu kulegea. Unahitaji Vitamini zaidi vya kiroho kuyakaza, Vitamini za tai, hilo ni Neno. Yakazeni hayo manyoya.

191 Ndipo jambo la kwanza atakapoyatoa yote, basi hana budi kuwafanya wamwamini, kwa hiyo anatandaza mabawa yake makubwa mno, na kupiga mayowe kwa sauti yake yote, anawapepea namna *hiyo*, huo upepo wa nguvu ukienda kasi, mwajua, unaoshuka. Loo, jamani!

192 Nao hao tai wadogo wanarudi tu nyuma. Hawaangalii nje, waseme, "Hebu tuone kile Dk. Jones alisema kulihusu." La, la, wanaangalia juu. Loo, nao wanayaona hayo mabawa makubwa mno. Mnaona, anajaribu kufanya nini? Anajaribu kuwafanya hao vifaranga wa tai watambue jinsi alivyo mkuu, zile nguvu, hawana budi kutumainia hayo mabawa makubwa.

193 Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, Yeye hupeperusha manyoya yote kutoka kwako, halafu ana mabawa mawili, Mungu anayo, mnajua hilo? Yehova-Tai. Hayo ni Agano Jipya na la Kale. Anayapepea mbele zako. Loo, jamani! "Mimi ndimi Mungu wa Musa. Mimi ndimi Mungu wa Ibrahimu. Mimi ndimi Mungu aliyemfufua Lazaro kutoka kaburini. Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa na ni hai tena, ni hai milele."

194 Agano Jipya na la Kale, akiyapepea huku na huku, maskini hao tai wadogo wamelala kule nyuma, wanasema, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!"

"Niaminini Mimi."

195 Inafaa nini kumpa kurumbizi vitamini kwa ajili ya mabawa yake, na kufanya mifupa mizuri, na mabawa, kisha kumweka kwenye kizimba? Inafaa nini kuwaelimisha wahubiri wa theolojia, na historia, na kadhalika, na kisha uwaambie siku za miujiza zimepita, na kuwaweka kizimbani katika madhehebu fulani? *Piiu!* Upuuzi! Mwachilie na umwache aruke, kama yeye ni tai. Amina. Sawa. Mwambie siku za miujiza zote zimepita, huyo si tai, huyo ni mwewe, naam, bwana, anayekula mizoga.

196 Sasa, angalieni kilichotukia, ndipo mama anapowafanya waone hao tai wadogo wamelala huko nje, na kusema, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi ulivyo mkuu!"

197 Je, uliwahi kutoka nje usiku na kuangalia? Nilikuwa hapa nje kwenye Mlima Palomar, naamini ndio. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuzunguka kote Beaumont. Bado haingekuwa imevunjiwa katika maili, na zaidi ya hapo. Naye alifanya nini? Ni "*Whiu!* tu" akawalipua kutoka mikononi Mwake. "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!"

198 Mwangalieni Mungu wa Musa, aliyeifungua Bahari ya Shamu, akawachukua wana wa Kiebrania katika tanuru iliyowaka moto, Danieli kutoka katika tundu la simba, Lazaro kutoka kaburini, "*Mimi* nina nguvu," Mungu alimfufua, hiyo ni kweli, lakini Yeye alisema, "*Mimi* nina uwezo wa kuutoa uhai Wangu, *Mimi* nina uwezo wa kuutwaa tena." Amina. Jinsi Wewe ulivyo mkuu! "Niaminini Mimi, MIMI NIKO yeye yule jana, leo, na hata milele."

199 Hizo mbawa kubwa, unaona ya kwamba Yesu wa Agano Jipya ndiye Yehova wa la Kale. Hizo mbawa kubwa zikipepea juu chini, huo upepo wa nguvu ukienda kasi, ukila huo. Loo, jinsi ninavyopenda kukaa katika upepo huo! "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Kuchochea kiota, naam, bwana, kujiweka tayari.

200 Ndipo siku moja anaamua, ni siku nzuri, ya samawati, kwa hiyo anaamua kuwachukua maskini wanatai wake kwenye safari yake ya kwanza. Tayari wameisoma Biblia yao yote, nao wanaona jinsi alivyo mkuu, yeye ni kama tu alivyowahi kuwa, mbawa zake kubwa, manyoya yake makubwa, ameandaliwa kuwatunza watoto wake. Kwa hiyo anatandaza mbawa zake, anajilaza nyuma namna *hiyo*, anasema, "Rukeni, enyi watoto."

201 Loo, nina furaha sana haikubidi kuirukia kanuni fulani ya imani, unarukia msalaba. Amina. Ninapomwona akitandaza: "Sina cha mikononi ninacholeta, ninakutumaini Wewe, Bwana, sijui jinsi nitakavyofanya jambo hilo."

202 Watakaponifukuza kutoka kanisa la Kibaptisti, "Sijui nitakalofanya, sijui, Bwana, bali nitaushikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Sijui utakavyolifanikisha, lakini, Mungu, Wewe umenichagua, ukaniambia niende nikawaombee wagonjwa. Wananiambia wataniweka katika hospitali ya wendawazimu

katika majuma machache, lakini jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!"

"Unaenda wapi?"

"Sijui, popote tu aniongozapo."

Yule ndugu aliyeniweka wakfu kanisani, alisema, "Unajua utaishia wapi?"

Nikasema, "Siku moja Utukufuni, bali ninaushikilia msalaba, ninamshikilia Mungu."

203 Mama tai anasema, "Rukeni sasa." Nanyi mnapaswa kuwaona hao jamaa wadogo, jinsi wanavyoshikilia. Wanachukua maskini makucha yao, na wanaona konzi zuri la manyoya namna *hiyo*, wanashikilia chini na kuchukua mdomo wao mdogo, wanaunyosha chini, wanakamata unyoya mwingine, wanasema, "Vema, Mama, niko tayari." Hmm!

Anaondoka kwenye kiota hicho, yuko juu sana hewani, kwa vyovyote vile, mnaona, maana wao si koho sasa, wao ni tai, wamezaliwa huko juu.

204 Usizaliwe *huku* chini, zaliwa *Huko* juu. Umezaliwa *huku* chini, wewe ni ndugu wa kimadhehebu, hiyo ni sawa, wewe ni ndege, pia. Lakini kama umezaliwa *Huku* juu, ndugu, umezaliwa katika Roho wa Mungu, haleluya, hujazaliwa kwa kanuni fulani ya imani, uko *huku* juu sana hewani.

Maskini mama anaruka kidogo namna hiyo, naye anayaweka hayo mabawa makubwa, wakati upepo unakuja vizuri tu, anapanda juu *sana*, anapanda juu.

Maskini tai mdogo, ninaweza kumsikia akiangalia kule, akisema, "Ndugu Jones, unaonaje kuhusu hilo? Loo, hili si ni zuri sana?"

"Hmm! Inanifaa vizuri kabisa. Sivyo?"

"Naam, bwana. Um-hum."

205 Akishikilia moja kwa moja, loo, jamani, kuendelea, kuendelea, kuendelea, kuendelea, kuendelea, mpaka asionekane tena pamoja na hao jamaa wadogo. Vema, kama hao walikuwa ni koho wangeanguka kitambo, wangalikuwa ni kunguru au hata mwewe, hawana budi kuwa tai la sivyo hawawezi kuvumilia. Wanajaribiwa kabla ya kufanya hiyo safari, hiyo ndiyo sababu hatufanyi safari nyingi sana. Whiu! Hmm! Sikupaswa kusema hivyo, labda. Lakini tayari imesemwa, kwa hiyo . . .

206 Kwa vyovyote vile, loo, wanapofika huko juu kabisa, mnajua anafanya nini anapofika kule juu? Je, yeye huangalia, na kusema, "Mmefanya vizuri sana, watoto, nitawarudisha moja kwa moja kwenye kiota chenu tena"?

207 La, bwana, yeye huwatupa, kila mmoja, nje. Wao ni tai, wanaweza kuruka, kama wao ni tai, *wanaweza* kuruka. Amina. Wao ni tai. Wanaweza kuruka kama wao ni tai. Anawarusha

nje, na kuruka anawaacha, anawaacha tu peke yao. Hao hapo juu hewani, ndugu, geuka tu, pigapiga, geuka, pigapiga, geuka, pigapiga, papaptika.

"Pigenipigeni kwa nguvu zaidi, enyi watoto. Endeleeni tu kupigapiga maskini mabawa yenu, ninyi ni tai."

208 Wanafanya mkutano wao wa Kipentekoste, wakipinduka tu tena na tena, wakiwa tu na wakati mzuri sana huko angani, amina, mbali sana na hao kuku wa kimadhehebu, huko juu kabisa angani, haleluya, huko juu kabisa angani, wakipigapiga tu huku na huku wakiwa na wakati mzuri sana.

209 Sasa, mnajua ni kwa nini wana wakati mzuri jinsi hiyo? Hawaangalii chini duniani. Jamani, hilo linaleta hisia nzuri. Jamani, wako huko juu mahali pao. Mkristo yeyote aliyezaliwa mara ya pili anapenda kuingia katika mazingira hayo huko juu. Nanyi mnajua ni kwa nini? Mama, yeye huinama upande mmoja, anashika hayo mabawa makubwa na kuwaangalia.

210 Loo, wana—wana imani kamili na mama yao. Nami pia. Mnaona? Loo, Yeye aliyenileta hapa juu, Yeye atanishughulikia. Yule aliyetoa ahadi, Yeye anaweza kutimiza ahadi Yake. Naye mama, uwezo wake wa kuwashika tena!

211 Kama ikitokea kwamba mmoja ametoka akakiuka utaratibu, mwajua, wanasema, "Huo ni moto mwingi sana wa kigeni." Afadhali niwe na moto mdogo wa kigeni kuliko kukosa kabisa. Angalau una nafasi ya kutosha kupigapiga mabawa yako. Kwa hiyo kama mmoja wao akienda shaghalabaghala, hawajali hilo, mama anamwangalia, anaona hatatoka humo, yeye hushuka tu kwa nguvu, anamchukua juu ya mbawa zake, na kumrudisha kwenye neema tena. Hilo ni fundisho zuri la Kikalvini, lakini, ndugu, hilo ni zuri. Kweli, inawaleta moja kwa moja kwenye neema tena, anambeba.

212 Anamweka kwenye mbawa zake za Neno, anasema, "Hapa, Mpenzi, umeondoka kwenye Neno sasa, unaenda kombo. Anarudi na kumjaribu tena sasa."

213 Anachukua Neno la Mungu na kumrudisha moja kwa moja kwenye neema tena. Amina. Loo, wana imani. Wanaamini, ndugu, wana wakati mzuri sana, wakipigapiga tu, na kupiga mayowe, na kupiga makelele, na kupaza sauti, wakiwa na mkutano wa kawaida wa Kipentekoste.

214 Sasa, hao kuku huko chini hawajui hata jambo moja kuhusu hilo, wanaangalia kule juu, na kusema, "Hayo yote ni ya nini? Sijawahi kusikia kitu kama hicho." Endelea, kaa ardhini ukitaka. Naam.

215 Mnajua, ilisemwa wakati mmoja ya kwamba mkulima alikuwa anaenda kumwatamisha kuku. Hebu tuone, huatamishwa mangapi? Kumi na matano? Nafikiri. Kumi na matano ni ya kuatamishwa kuku. Ninamsikia maskini

mama fulani mzuri huko nje akisema, “Ndiyo.” Ninakumbuka Mama alikuwa akiweka alama za penseli kila mahali, ili aweze kujua kama kuna yai jipya mle ndani au la, mwajua. Ilitubidi kuangalia jambo hilo. Unaona? Yai jipya lilimaanisha jambo fulani. Kwa hiyo angemwatamisha kuku, kumi na matano.

216 Naye huyo mkulima alikuwa na mayai kumi na manne tu. Kwa hiyo akapanda juu ya jabali na kuchukua yai la tai, akalileta chini, akaliweka chini ya huyo kuku. Wakati lilipoanguliwa, kulikuwa na kuku kumi na wanne na tai mmoja. Hiyo ni kama ndiyo wastani, mmoja kutoka kwa uatamishaji. Hiyo ni kweli. Hivyo karibu ndivyo wanavyofanya, yapata mmoja katika uatamishaji.

217 Kwa hiyo, wakati maskini tai huyu alipozaliwa, ungeweza kuwazia jinsi alivyokuwa bata wa kipekee katika dhehebu hilo huko chini. Mbona, hakuelewa kile kuku huyo mzee alikuwa akienda—akizunguka-zunguka, kusema, “*Chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi!* Sasa, mnaona siku za miujiza zimepita. *Chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi!*”

Akasema, “Kuna nini?”

218 Alitoka huko nje na kukwaruza-kwaruza, mwajua, kwenye kitalu hicho, “Nitakuwa na mlo wa supu jioni usiku wa leo, ninyi nyote hudhurieni,” mwajua, yote namna hiyo.

219 Mbona, hakujua, hakupenda chakula cha namna hiyo, hicho kilimtia kichefuchefu. Wote walimdhihaki. Loo, sote tumekuwa na tukio hilo, sivyo? Kutufanyia mzaha. Ninawazia maskini hao tai wa kike, kulikuwa na *kitu fulani* kumhusu, wala hakuwa na mabawa mafupi, yaliyokatwa, alikuwa na mabawa marefu, maana alikuwa . . .?. . .

220 Hmm! Sitaki kuwaudhi, ninawapenda sana. Lakini, ndugu, wakati mwingine unapapasa manyoya kinyumenyume kidogo mara moja moja ili kukusaidia.

221 Kwa hiyo, akazunguka, mwajua, katika maskini mabawa yake madogo, kasema, “Vema, mbona—mbona mimi sifanani na hao wengine? Ni kwa nini siwezi kujifurahisha katika mambo kama hayo? Mbona hivi?”

222 Vema, wewe ni kiumbe tofauti tu, hivyo tu. Unaona? M—mlikuwa . . . Tulikusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kuwa tai, si koho, wala kuku. Mnaona?

223 Akitembea pale, mwajua, maskini yule kuku alikuta, huko nje kwenye lundo la samadi, ataanza kuchakura maskini mizoga ya ulimwenguni, akisema, “Sasa, tutakuwa na mashindano ya mbio za duara huko chini ufukoni, ambako wote wanaenda kuogelea.”

“Jamani, masalale! Hmm!” Nisingeweza kuvumilia hilo.

“Tutakuwa na mchezo wa karata kwenye orofa ya chini.”

“Hmm?” Maskini huyo . . .

224 Bingo, hivyo ndivyo ilivyo, bingo. Ninaninii tu, sijui majina ya namna hiyo. Vema. Banko ni nini? Ndivyo? Mimi, labda nilikosea. Bingo, unaona, chochote kile. Hata hivyo, “Tutakuwa na hiyo.”

225 Maskini tai huyo mdogo asingeweza kuelewa hilo, hicho hakikuwa kitu alichokuwa akila, hakikumkaa sawasawa. Je, ulijisikia hivyo ulipokuwa huko nje? Jamani, nilijisikia hivyo. Jamani! Mambo hayo yalivunda kwangu. Ati mnajiita Wakristo? Mchungaji hana budi kusimamisha kanisa dakika kumi na tano mapema apate kuvuta sigara kabla hajarudi mimbarani; halikusikika sawa kwangu. Mashemasi wote walikimbia kule, na—nami nilijua wanatembea na wanawake kanisani, na mambo kama hayo, hilo halikusikika kama Wakristo kwangu mimi. Mnaona? Kamwe halikutoshea sawa.

226 Kwa hiyo akatembea huku na huku. Ilibidi awe nyuma wakati wote. Kamwe hawatakuweka katika chochote, usiwe na wasiwasi kuhusu hilo. Kwa hiyo kamwe . . . Hawana budi kwenda huko nje ambako wanaonekana kama kuku, mwajua. Kwa hiyo muda si muda mwajua, akatembea kila mahali. Yeye—yeye kwa kweli alikuwa—alikuwa ni—alikuwa namba ya kipekee. Na Mkristo yeyote aliyezaliwa mara ya pili katika mchafuko kama huo, tai yeyote mahali kama hapo ni namba ya kipekee. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hakujua la kufanya, maskini jamaa huyo hakujua vizuri zaidi. Labda hatukujua. Hatukujua vizuri zaidi.

227 Na siku moja mnajua nini? Mama alijua alitaga mayai mawili, mvua ya masika, na mvua ya vuli. Ilikuwaje kwa moja la hayo? Kwa hiyo akaanza kumtafuta. Huyu hapa anakuja, akipigapiga mbawa hizi, alikuwa akiangalia pande zote kwa hayo macho yenye kupenya, angeweza kuangalia kila mahali. Akaruka juu ya kitalu, aliporuka akasema, “Mwanangu!” Hilo halikusikika, “*Chwi*, *chwi*, *chwi*.” La.

Akakigeuza maskini kichwa chake na kuangalia juu, kasema, “Hiyo inasikika halisi. Hiyo ilitoka wapi?” Loo, jamani!

228 Unakumbuka mara ya kwanza Mungu aliponena nawe? Loo, utukufu! Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali tu muanze sasa. Loo, jamani! Nilipoisikia Sauti Yake kwa mara ya kwanza ilinena kama maji mengi. Loo, jamani! Karibu na kijito *kidogo*, ama, kijito cha viwimbi, ili aweze kulala chini, kuoga, kuangalia juu. Jamani!

Akaangalia juu, na kusema, “Hiyo ilikuwa ni nini?”

Akarudi, akasema, “Mpenzi, wewe ni wangu! Wewe si wa mahali hapo, kwa vyovyote vile.”

229 "Toka kati yao, ukatengwe nao, asema Bwana, usiguse vitu vyao vichafu, nami nitakuwa Mungu kwako. Nitakuwa Mungu kwako, utakuwa mwana na binti Kwangu." Mnaona?

"Wewe si mfuasi wake, madhehebu hayo ya kale yanasema siku za miujiza zimepita. Wewe ni wangu, wewe ni tai." Unaona?

"Loo, hilo linasikika zuri," akasema. "Ninaelewa mazungumzo ya namna hiyo."

230 Naam, bwana. Kwa nini? Kwanza kabisa yeye alikuwa ni tai. Kwa kweli alikuwa ni tai, aliingia tu kwenye kiota kisichofaa, hivyo tu. Natumaini siwaudhi ninyi ndugu, lakini ni—ninawaambia tu ukweli. Hiyo ni kweli. Wengi wao siku hizi wako kwenye kiota kisichofaa.

"Loo," kasema, "ati katika kiota kisichofaa, aha, Mama? Hicho ndicho kilichotendeka?"

"Naam."

"Hivi wewe ni Mama yangu?"

"Naam, mimi ni baba yako, na mama, dada, ndugu pia. Mimi ni yote kwa yote kwako."

"Hilo linasikika zuri, Mama. Sasa, Mama, nifanye nini?"

231 Kasema, "Nakwambia, Mpenzi, kile unachopaswa kufanya, huna budi kuruka. Huna budi kuruka, uindoe miguu yako ardhini, halafu basi uanze kuyapigapiga maskini hayo mabawa yako, yapige tu kwa nguvu uwezavyo. Unaweza kuinuka, maana wewe ni tai. Unaona, una manyoya marefu. Ruka! Ruka tu kutoka ardhini, na uanze kupigapiga mbawa zako kwa nguvu sana, nitakushika."

232 Naye akaruka juu, maskini tai huyu akitoka kwenye hayo madhehebu, na kupigapiga mbawa mara nne au tano, na kutua moja kwa moja kwenye nguzo ya kitalu, moja kwa moja katikati ya madhehebu ya Kipentekoste.

233 Huwezi kuiundia Pentekoste dhehebu, huwezi kuifanya dhehebu, Pentekoste ni tukio, si dhehebu, ni kwa ajili yenu Wamethodisti, ninyi Wabaptisti, ninyi Wapresbiteri. Wanajaribu kuizungushia nyua, lakini sivyo ilivyo, tai wataruka moja kwa moja juu yake. Hakika, wanaruka, hawalijali.

Mama pitia hapa, akasema, kasema, "Mama, si ninaendelea vizuri? Angalia mahali nilipo sasa, Mama!"

Akasema, "Mwanangu, itakubidi kuruka juu zaidi ya hapo, la sivyo hata siwezi kukushika."

234 Hapo akaruka tena kwa kasi sana. Akarusha miguu yake midogo hewani na kuanza kupigapiga mbawa zake kwa nguvu alivyoweza, basi muda si muda mwajua, akajisikia akiinuliwa juu, juu, juu, mpaka akaifikia ile Njia ya Kilimia Cheupe. Amina. Ndipo angeweza kuruka mwenyewe, baada ya kufika juu vya kutosha, angeweza kuruka mwenyewe.

235 Ndugu, hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, kamwe halijapata kuinuka juu vya kutosha, lipate tu kutoka kwenye madhehebu ama *kitu kingine*, lipate kuona kama lingeweza kuruka au la. Naam, bwana. Unajuaje huwezi kuruka? Tumia mbawa zako. Haleluya! Ruka ndani yake, uanze kupigapiga mbawa zako upate kujua. Yehova atakushika. "Nitamchukua kwa mbawa za tai." Amina. Loo! Whiu! Jamani! Jamani!

> Ninakuta watu wengi ambao hawawezi kuelewa
> Kwa nini tuna furaha sana na huru;
> Nimejazwa na Roho, hapana shaka,
> Na hiyo ndiyo shida yangu.

Naam, bwana. Loo, jamani!

> Tumevuka Yordani tukaingia katika nchi nzuri ya Kanaani,
> Hii ni kama Mbinguni kwangu.

236 Hiyo ni kweli, ndugu, dada? Hivi huna furaha wewe ni tai leo? Yehova-Tai pamoja nasi, Mungu, Yehova-Tai, Yeye yu pamoja nasi. Ninampenda, nanyi je? Na tuinamishe vichwa vyetu. Aliniambia tu jambo fulani wakati uo huo.

237 Ni wangapi hapa ndani wangetaka kuruka mbali na kiota cha kale cha mwewe, utoke uingie katika Kristo, na uishi huru katika Roho? Inueni mikono yenu, na kusema, "Niombee, Ndugu Branham." Loo, angalia tu hiyo mikono! "Heri wenye njaa na kiu." Huenda huu ulikuwa ni ujumbe mbaya sana, kanisa. Ni fidhuli kwa sababu sina elimu, mimi si mwa—mwanatheolojia. Maskini njia fidhuli tu za jinsi nilivyoyaangalia maumbile, na kujua Mungu aliyaweka maumbile. Kwa hiyo, Yeye—Yeye ni Mungu, Yeye—Yeye ni—Yeye angali hapa, Yeye—Yeye anajua mambo yote.

238 Iweni tu katika, kimya cha dakika moja. Na—nataka kuona kile anachotaka nifanye. Iweni tu katika maombi, "Bwana, unirehemu. Niliinua mkono wangu, shika mkono wangu, na kuniinua juu ya kivuli sasa hivi."

239 Hmm! "Jinsi Wewe ulivyo mkuu, jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Yeye si ni wa ajabu? Ogeni tu sasa, huu ujumbe unakata na kuchubua, ogeni tu katika utamu Wake.

> Jina tamu kuliko yote katika lugha ya mwanadamu,
> Wimbo mzuri kuliko zote uliowahi kuimbwa,
> Loo, Yesu, Yesu mbarikiwa.

240 Omba tu sasa, kimyakimya moyoni mwako. Acha Roho Mtakatifu aingie moja kwa moja nafsini mwako. Sema, "Bwana, nichukue jinsi nilivyo." Mnaona, hakuna kitu ninachoweza kufanya sasa, Yeye hana budi kufanya hayo mengine, mnaona. Omba tu, useme, "Baba," omba tu kimyakimya moyoni mwako,

jinsi unavyotaka kuomba, wewe uliyeinua mkono wako, sema, "nipokee sasa, Bwana Yesu. Ninataka kuwa tai, ninataka kuruka niende katika utukufu wa Mungu, niwe katika nguvu Zake."

Ndiyo:

Kuna Chemchemi,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini ya hiyo gharika,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

241 Ombeni tu sasa. Hmm! Ni tukufu jinsi gani! Hivi hampendi tu kuhisi huko kuoga? Hili ndilo ninalozungumzia. Nimesimama tu hapa, vidole vyangu vimeinuliwa, na mikono yangu imekazwa sana, Roho wa Mungu akitenda kazi jengoni.

242 Ninaliacha lizame chini kabisa, kusudi watu waweze kuwazia kwa dakika moja tu. Wazieni mawazo haya: "Mimi ni nani? Hivi ninajua nitaishi siku hii yote? Nitaenda wapi Mungu akiyachukua maisha yangu? Ninajua kweli ya Mungu sasa." Amina. Hebu wazia tu.

243 Mtazamo mzuri sana! Fungeni macho yenu, ninaangalia tu kitu fulani humu jengoni, naona utakatifu, Mungu akifanya kiota Chake sasa mumo humo chini moyoni mwako, akilileta Neno sasa, akiliweka humo: "Yesu Kristo yeye yule jana na hata milele," akiyaweka hayo kwenye kiota moyoni mwako. "Mimi Ndimi aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja," akiyaweka hayo kwenye kiota moyoni mwako, unaona.

Jinsi Wewe ulivyo mwema! Mnampenda?

Kisha katika wimbo mzuri zaidi, mtamu zaidi,
Nitaimba ninii Yako . . . ya kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kitembe,
Utakapolala kimya kaburini.

244 Sasa, ninyi mnaomhisi, na mnaojisikia ya kwamba amewekwa kwenye kiota, na ameweka baadhi ya Maneno, na kitu fulani moyoni mwako ambacho unajua unaweza kutoka hapa ukiwa mtu bora zaidi, unajisikia ya kwamba una vitamini za tai moyoni mwako sasa ambazo zitakufanya tai, mnyoshee mkono wako kwa urahisi sana, hiyo ni sawa, useme, "Ninaamini, Bwana, utanifanya tai kwa neema Yako, sistahili, bali mimi ni tai Wako tangu sasa na kuendelea." Mungu awabariki. "Ninaweza kuruka, sijali nini, mradi tu ninaangalia Neno Lako kuu hapa, na kusema, 'Wewe ni yeye yule, ninaamini Wewe ni yeye yule, ninakuamini Wewe kwa moyo wangu wote.'"

245 Hisia hiyo tamu! Ndio kwanza nione, akija moja kwa moja, moja kwa moja kunielekea mimi, anakuja Malaika wa Bwana, ile Nuru. Ninajua alikuwa hapa mahali fulani, yuko karibu na hili jukwaa sasa. Ninamchukua kila mtu hapa ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu

wa Mungu. Ninawatakeni mwe na imani sasa ya kuamini. Msiwe na shaka, iweni na imani. Sasa inua kichwa chako, kwa urahisi sana, sasa angalia huku.

246 Yehova-Tai, nguvu Zake kuu! Mwanatai ni mzao Wake. Hiyo ni kweli? Mambo ambayo baba tai hufanya, maskini mwanatai wake hufanya vile vile. Hiyo ni kweli? Kama Yehova-Tai, basi mwanawake Wake tai (Mnaona ninalomaanisha?), binti Yake tai, wote ni sawa. Hiyo si ni kweli?

247 Nakisia kulikuwa na angalau mikono arobaini, hamsini, au zaidi, iliyoinuliwa dakika chache tu zilizopita, kwa ajili ya wokovu. Kabla sijawaomba wasimame, Roho wa Bwana anaingia humu jengoni sasa hivi. Nilikuwa nikimwangalia moja kwa moja *hapa* nyuma mahali fulani, katika sehemu ile *pale*, alikuwa akisogea, akaendelea kujongea *huko*, kisha akajongea juu, akavuka jukwaa, akashuka na kwenda upande *ule*, halafu nikamwona akipotelea nyuma *hapa* ndani, na halafu akarudi moja kwa moja *huku* tena, akazunguka juu ya hili jengo moja kwa moja.

248 Sasa, usiniambie sijui ninalozungumzia, ninajua, ninajua ninalozungumzia. Yuko hapa. Ninaamini alichomaanisha kwa jambo hilo, kwamba alikuwa akilizunguka kusanyiko lote. Hiyo ni kweli. Yeye—Yeye anawapenda, a—anawataka, anawataka mumtumikie Yeye. Yeye—Yeye. . . Wewe ni wake, Yeye ni wako, Yeye ni Bwana wako, Mwokozi wako. Sasa, kuna jambo moja tu unaloweza kufanya, na hilo ni kuamini, hilo tu, hilo ndilo jambo pekee unaloweza kufanya, unaamini, na kisha Mungu anaithibitisha imani yako kwa kukupa Roho Mtakatifu.

249 Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kwamba ana haki, bali Mungu alimpa muhuri wa tohara kuithibitisha imani yake. Maadamu hujampokea Roho Mtakatifu, huenda ukawa na imani, hiyo ni kweli, bali Mungu hajaithibitisha bado. Na wakati umetiwa muhuri, umetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wako, Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Hilo si ni zuri sana? Naam. Sasa, Yeye haokoi tu. . . Haponyi tu, bali anaokoa.

250 Ninamwangalia Roho huyo anapotembea. Sasa, inakubidi kuwa katika hali fulani, hakika, sisi sote hatukuumbwa hivyo, hiyo ni kweli kabisa. Ilikuwa hivyo katika Biblia, hakika ilikuwa hivyo, mnaona, daima. Lakini nilikuwa nikimwangalia. Sasa amerudi tena, ninamwangalia moja kwa moja sasa, Huyo *hapo* tena.

251 Ninii tu, wewe sema neno linalofaa, sema tu jambo linalofaa, ni kile unachosema. Ni wangapi waliosoma hicho kitabu, ama, nadhani liko kwenye kanda, ambapo huduma hii mpya, ninii tu, mwanamke huyo alisema tu jambo linalofaa? Nikasema, "Omba

lolote utakalo sasa, uone kama Mungu atalifanya. Atakupa sasa hivi. Sijali . . . ”

Kasema, “Niombe nini, Ndugu Branham?”

252 Nikasema, “Chochote unachotaka.” Nikasema, “Huyu hapa dada mlemavu ameketi; baba na mama yako ni maskini; huna pesa zozote; wewe ni mjane. Unataka nini?”

Akasema, “Chochote?”

253 Nikasema, “Tafuteni kujua kama ni kweli ama si kweli.” Hiyo ndiyo ile huduma mpya inayokuja, nimesimama hapa kwa dakika kumi na tano, ishirini nikiingojea. Mnaona? Sema tu utakalo, unaona, Yeye hana budi kuniambia kwanza.

Nikasema, “Dada Hattie, sema tu chochote utakacho.”

Akasema, “Shauku kuu ya moyo wangu ni wavulana wangu wawili matineja, pale, ili wapate kuokolewa.”

Nikasema, “Ninawakabidhi kwako, katika Jina la Yesu Kristo.” Wakaangukia pajani mwake, papo hapo. Mnaona? Loo, ni mambo ya jinsi *gani* yaliyotukia!

“Kama unaweza kuamini!”

254 Mama huyu aliyeketi papa hapa, papa hapa nje, akiomba, ameshikwa na fadhaa, hakuna tumaini kwake, hawadhani. Anatoka Mississippi. Sawa. Ili uweze kujua, baba yako ni mgonjwa, pia, sivyo? Yeye ni mhubiri, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ninakukomboa, katika Jina la Yesu Kristo, kutokana na fadhaa hiyo. Nenda, nawe umeponywa, Bibi Hansen.

Sijawahi kumwona maishani mwangu. Mwulizeni ikiwa mambo hayo si kweli.

Ni ya kweli, mama? Punga mkono wako, kama hiyo ni kweli. Hatufahamiani? Punga mkono wako.

Aligusa nini? Ni kitu gani? Loo, jamani! Yeye yule jana, leo, na hata milele. “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya.” Je, ninyi ni waaminio?

255 Huwezi kulala unapoenda nyumbani kutoka, usiku, kutoka kanisani, sivyo, mama? Ninakuona umelala pale, ukigeukageuka, ukisogea. Jana usiku ulikuwa na usiku mbaya sana, sivyo? Sawa. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, ama, mtumishi? Unaamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Vema. Kama unaamini namna hiyo, nifanye nini nipate kukusaidia? Kama nikikwambia—kama nikikwambia, umekombolewa, unaliamini? Mahali palipokuwa na giza juu yako, pameingia nuru. Jina lako ni Bibi Heuser. Vema, unaweza kurudi nyumbani, ukaponywe. Yesu Kristo . . .? . . .

256 Mama, wewe uliyeketi karibu naye, ulikuwa mwema sana kwa kumgusa kumfanya ajue kwamba ilikuwa ni yeye. Si ulikuwa ukimgusa mama huyo, ukimwambia? Nilifikiri ulikuwa

ukimwambia kuhusu . . . Vema, una jambo fulani niani mwako, kwa hiyo kama wewe . . . Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu atatenda huo mwujiza? Vema. Huyo mlevi sugu ataponywa, kama utaamini kwa moyo wako wote. Umekuwa ukimwombea ndugu yako kwa muda mrefu.

Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, jamani, huku si kuigiza kanisa, hizi ni nguvu za Bwana Mungu.

Hapa, huyu hapa mama mzee ameketi, akiangalia kule, hawezi kuelewa haya yote yanahusu nini hasa, mama huyu aliyeketi papa hapa nyuma.

257 Hiyo *hapo*, inaning'inia ile . . . Huwezi . . .? Na—najua, hakuna haja ya kukuuliza jambo hilo. Ninaiangalia hiyo Nuru, imening'inia moja kwa moja juu yake.

258 Anateseka, ni mgonjwa, ana ugonjwa wa figo, ugonjwa wa moyo. Anakosa, sasa ku- . . . Bibi Weir, amini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki. Simama kwa miguu yako, na uponywe.

259 Sasa, kama sikujui, nawe hunijui, punga mkono wako huku na huku, ili watu wajue. Je, kila kitu alichokwambia kilikuwa ni kweli? Kama hiyo ni kweli, punga . . . Simama kwa miguu yako ili watu wajue ya kwamba hiyo ni kweli, kama kila kitu kilisemwa kweli, na mimi na wewe hatufahamiani.

260 Haleluya! Toka uingie angani, na kupigapiga mabawa yako. Amina. Haleluya! Vipi kuhusu hilo? Je, wewe ni tai? Uko tayari kuruka? Kama uko tayari kuruka, simama kwa miguu yako, na kudai uponyaji wako, na wokovu wako, na kila kitu kingine unachohitaji, sijali kuna shida gani. Njoni, enyi wana tai, inukeni mruke mkaondoke kwenye dhehebu hili hapa la kuku wa duniani.

261 Bwana Mungu, Ee Mungu wa Mbinguni, tuma Roho Wako na nguvu Zako ndani ya kila mmoja, katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . .

61-0122 Mfano Wa Tai Ataharikishavyo Kiota Chake
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org